# Nipashe

Jumamosi Aprili 10, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580546

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US





UKURASA 11

**Mwekezaji** afungwa miaka 30 kwa kuzalisha bangi

UKURASA 4



**Naibu** Waziri anusa ufisadi ujenzi maabara

UKURASA 4

# Mauaji ya kinyama

• **Mume** na mke wauawa, miili yakutwa kichakani, mwanafunzi wa miaka 10 abakwa hadi kupoteza maisha... *Endelea ukurasa 2*




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akishiriki katika mkutano wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), unaozungumzia masuala ya Ulinzi na Usalama wa nchi wanachama wa jumuiya hiyo, jijini Maputo, Msumbiji jana, akimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan. Nyuma yake ni Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula. **PICHA: IKULU**

## Ripoti ya CAG yaibua mawaziri

UKURASA 3

## Wabunge wakoleza moto mjadala kuboresha biashara

UKURASA 2


**MICHEZO** **YANGA SC YAIANDALIA DOZI KMC** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akijadiliana jambo na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama (katikati) na Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira, Patrobas Katambi, Bungeni jijini Dodoma, jana. **PICHA: OWM**

# Mume na mke wauawa kinyama

**Na Elizabeth John,** NJOMBE.

MUME na mke, wakazi wa kijiji cha Itulike, Kata ya Ramadhani, Halmashauri ya Mji wa Njombe, Nicodemus Ng'ande na Renatha Mtega, wameuawa kinyama kasha miili yao kutupwa vichakani.

Kutokana na mauaji hayo, yaliyofanyika Machi 19 na 20, mwaka huu, watu tisa wanashikiliwa na jeshi la polisi mkoani Njombe kwa tuhuma za kuhusika na matukio hayo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Hamisi Issah, alisema watuhumiwa hao ambao majina yao hawakuyataja kwa kuwa upelelezi unaendelea ili kubaini wengine zaidi, wanaodaiwa kufanya mauaji ya Renatha (60) na Ng'ande (60).

Alisema Mtega aliuawa Machi 19, mwaka huu, na mwili wake kutupwa katika msitu wa TANWAT na Ng'ande alifanyiwa kitendo hicho siku iliyofuata na kutupwa eneo la Maheve na mwili wake kufunikwa na turubai.

Mauaji hayo, Kamanda Issah alisema, yaligundulika baada ya mtoto wa marehemu hao, Emmanuel Nicodemas, kufika akitokea Dar es Salaam na kukuta nyumba ya wazazi wake haina mtu hata mmoja.

Alisema alipoanza kufuatilia kwa kushirikiana na wanakijiji, waliupata mwili wa mama yake na hapo ndipo polisi walianza uchunguzi na kukamata watuhumiwa tisa.

"Hao watuhumiwa tisa walikaa kwenye mahabusu ya polisi na baadae katika uchunguzi ilibainika kuwa watu hao tisa ndio waliokaa na kupanga mpango wa kuua," alisema.

Pia alisema katika mahojiano juzi, watu hao walikwenda kuonyesha mwili wa Ng'ande ukiwa unaonyesha kuwa aliuawa kikatili kwa kufungwa mipira ya baiskeli miguuni na mikononi na baadaye kufunikwa na turubai.

"Na lile Turubai lilipakiwa katika pikipiki kutoka Itulike hadi Maheve kwenye misitu ya TANWAT katika shamba la mipaini (pine trees). Mwili huo ulikuwa umebondeka maeneo ya kichwani," alisema Issah.

Kamanda alisema watuhumiwa hao waliwapeleka polisi na kuonyesha vifaa vilivyotumika kupasua kichwa cha Ng'ande ambavyo ni nyundo na sururu.

Alisema katika jambo ambalo si la kawaida, baada ya kurudi katika eneo la tukio, watuhumiwa watatu kati yao walitaja pikipiki iliyohusika kubeba mwili wa marehemu ambayo kwa sasa inashikiliwa na jeshi hilo.

"Isitoshe kuna watuhumiwa wengine watatu ni jamii ya marehemu Renatha Mtega kwani watumia jina la ukoo huo wa Mtega na wamesema wapo tayari kufa au kufungwa ili mradi familia zao zibaki salama. Hayo mambo wanasema waliambiwa na babu yao" alisema Issah.

## Mwanafunzi auawa atupwa kichakani

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

MWANAFUNZI wa darasa la nne katika Shule ya Msingi Kahororo, Manispaa ya Bukoba, Irene Revocatus (10) ameuawa kwa kupigwa na kitu kizito kichwani, kubakwa, kisha kutupwa kichakani na watu wasiofahamika.

Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Kagera, Revocatus Malimi, amethibitisha kutokea tukio hilo na kusema majira ya saa sita mchana Aprili 6, mwaka huu, mwili wa Irene uliokotwa kwenye kichaka kando ya Ziwa Victoria.

Malimi alisema Aprili 5, mwaka huu, Irene aliagizwa na mama yake mzazi, Agnes Salvatori (30), mkazi wa Mtaa wa Rwazi kwenda kununua sabuni dukani.

"Mahojiano zaidi yalibaini kuwa marehemu alikuwa anatumwa na kurudi haraka. Lakini siku hiyo alichelewa kurudi na baada ya masaa mawili ndipo mama yake majira ya saa 8:00 mchana, aliamua kumfuatilia hadi dukani na alipouliza akaambiwa hajaonekana kufika dukani," alisema Kamanda Malimi.

Alisema, duka hilo alilokuwa ameagizwa lilikuwa mbali kidogo na nyumbani.

Kamanda Malimi alisema mzazi huyo akifika kituo cha polisi Aprili 5, mwaka huu, kutoa taarifa ya kupotelewa na mwanawe na kurudi nyumbani kushirikiana na majirani kumtafuta na siku iliyofuata walimkuta akiwa ametupwa kichakani.

Baada ya kupatikana kwa mwili na kufanyiwa vipimo na daktari, ilibainika kuwa sababu ya kifo ni jeraha kubwa kichwani lililotokana na kupigwa na kitu kizito na alama za kubakwa.

# Wabunge wataka kamati kunusuru biashara

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MBUNGE wa Kinondoni, Abbas Tarimba (CCM), ameitaka serikali kuunda kamati maalum itakayojumuisha wataalamu na wafanyabiashara mashuhuri ili kuishauri serikali njia bora za kunusuru anguko la biashara nchini.

Alitoa ushauri wake huo alipochangia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26) uliowasilishwa bungeni jijini Dodoma juzi na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba.

"Kitu kimoja kimenitia moyo lakini kimenisononesha sana. Tuna watu wazuri sana katika nchi hii katika mawazo ya kufanya biashara. Nimpongeze mpinzani wangu Mohamed Dewji ambaye tumesikia ameteuliwa na Rais wa South Africa kuwa mmoja wa watu ambao watamshauri," alisema.

Mbunge huyo alihoji kama Tanzania ina watu wa namna hiyo ambao nchi zingine zinawaona, serikali inawatumiaje watu hao.

Tarimba alisema serikali imezungumza mambo mengi katika mpango huo na hivyo ni lazima serikali itakapokuja kufanya majumuisho, ilieleze Bunge namna ilivyojitayarisha kuhakikisha kuwa inaitumia sekta binafsi.

Alisema sekta binafsi ni miongoni mwa wabia wakubwa katika mpango huo ambapo Sh. trilioni 40.6 zimeainishwa kuwa zitatokana na mchango wa sekta binafsi na Sh. trilioni 74.2 zitatokana na serikali.

Mbunge huyo alisema ni lazima jumuiya ya wafanyabiashara iangaliwe vizuri na angependa kuona mchango wa serikali katika kuhakikisha jumuiya hiyo inalelewa vizuri.

Mbunge wa Manonga, Seif Gulamali (CCM), aliunga mkono hoja hiyo akisema Rais Samia ameanza vizuri kwa kushughulikia kero zilizokuwa zinawaumiza wananchi, lakini akatahadharisha kuwa bila kutengeneza mazingira rafiki kwa wafanyabiashara, fedha zitaendelea kutoonekana mifukoni mwa wananchi.

"Hakuna nchi inayoweza kukua kiuchumi bila kuwa na mazingira mazuri kwa wafanyabiashara. Hiki kinachosemwa fedha kutoonekana kwenye mifuko ya wananchi, ni matokeo ya biashara kuyumba.

"Mfanyabiashara asipopata faida, bidhaa za mfanyabiashara kama hazinunuliki, wanaoumia ni wananchi wa kipato cha chini kwa sababu wafanyabiashara hawatatoa fedha kuja huku chini.

"Kwa hiyo, kuna haja sasa serikali ikae na wafanyabiashara wakubwa hao kina Mo Dewji, izungumze nao ili kutatua kero zinazowakabili kwa lengo la kutengeneza mazingira mazuri ya biashara," alisema.

Mbunge wa Vunjo, Dk. Charles Kimei (CCM), aliitaka serikali kupunguza kukopa ndani ili kuepuka kudhoofisha taasisi za ndani kifedha. Mtaalamu huyo wa masuala ya uchumi na fedha pia aliitaka serikali kuhakikisha kuwa kabla ya uzalishaji wa bidhaa za kilimo, ijiridhirishe juu ya soko la bidhaa husika.

Mbunge wa Geita Mjini, Constantine Kanyasu (CCM), alisifu hatua zilizochukuliwa na Serikali ya Awamu ya Tano kwa kufanya marekebisho ya Sheria ya Madini, akibainisha kuwa matokeo chanya yameonekana mjini Geita.

"Ukifika mjini Geita leo, utaona namna maendeleo yalivyopatikana kutokana na marekebisho ya sheria hii. Tatizo ninaloliona limebaki ni kutozingatiwa kwa sheria katika uingizaji wa malighafi kutoka nje," alisema.

HABARI KITAIFA

## ... Mhagama aagiza mfumo mpya vibali kazi

**Na Augusta Njoji**, DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, amemuagiza Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Tixon Nzunda kuhakikisha mfumo wa utoaji wa vibali vya ajira kwa wageni unaanza kufanya kazi kabla ya mwisho wa mwezi huu.

Sambamba na hilo, Waziri Mhagama amewataka watumishi wa ofisi yake kutekeleza majukumu waliyokabidhiwa kwa ufanisi, kwamba hatosita kuwachukulia hatua.

Alitoa maagizo hayo jana wakati akizungumza na watendaji wakuu wa sekta zilizopo katika wizara yake jijini hapa, kueleza kwamba kuanza kwa mfumo huo kutasaidia kuondoa mianya ya rushwa.

"Katibu Mkuu nilishatoa maelekezo haya, siku iliyopangwa mawaziri kutoa mawasilisho ndiyo siku ambayo Rais alitupa mshangao wa mabadiliko ya baraza, lakini tangu hapo hakuna aliyekuja kuulizia, tulitakiwa tuwe tumeshazindua mifumo huo, sasa nataka nipate maelezo ni kwa nini mfumo huo hatuuzindui," alisema Mhagama na kuongeza;

"Zipo taarifa nazisikia kuwa bado kuna vitu vinakwamisha lakini wala siyo sababu ya kutufanya tusifanikishe jambo hilo la muhimu sana, sasa sijui anasubiriwa waziri au manaibu ndiyo waseme tena, huu siyo utaratibu mzuri, kila mtu asukumwe kufanya kazi, tuache utendaji wa mazoea, mimi ningependa mara tunapomaliza bajeti yetu, tumpe zawadi waziri mkuu kwa kuanzisha mfumo huu ambao unaenda kutatua kero,"alisisitiza Waziri Mhagama.

Waziri Mhagama alisema: "Tunajua wapo mawakala wengi wanakwenda kwa waajiri wakijifanya wanaweza kuwasaidia kupata vibali na wanachukua fedha na hapo inaonekana ofisi ya waziri mkuu, sasa ni vyema tujitoe kwenye hii taswira".

Aidha, aliomba kukutanishwa na maofisa rasilimali watu kwenye kampuni kubwa zote ili ajue changamoto zao na shida wanazopata.

Akipokea maelekezo hayo Katibu Mkuu Nzunda, aliahidi kuyatekeleza kwa kusimamia misingi mitatu ambayo ni weledi, uadilifu na bidii ya kazi.

Nzunda alisema: "Mimi siyo mtu wa mchakato napenda kazi itoe matokeo haraka na nitafanya hivi kwa kuzingatia katiba, sheria, taratibu na mifumo ya utendaji kazi".



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Justine Masejo, akiwaonyesha waandishi wa habari jana, baadhi ya dawa ya kulevya aina ya bangi, zilizokamatwa na jeshi hilo, katika operesheni maalum. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Ripoti ya CAG yawaibua mawaziri

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RIPOTI ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), iliyotolewa juzi, imewaibua mawaziri na kutaka hatua zichukuliwe katika maeneo ambayo yamebainika kuwa na kasoro.

Kutokana na ripoti hiyo, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imetoa maelekezo 10 kwa mikoa na mamlaka za serikali za mitaa ikiwamo kushauri mamlaka za uteuzi ya wakurugenzi wa halmashauri zichukue hatua stahiki.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Ummy Mwalimu, alitaja halmashauri nane zilizopata hati mbaya kuwa ni Itigi, Singida, Shinyanga, Momba, Igunga, Sikonge, Urambo na Manispaa ya Tabora.

Kuhusu Halmashauri 53 zilizopata hati yenye shaka, alisema mikoa yenye halmashauri nyingi na idadi kwenye mabani ni Dodoma (saba) Kigoma (sita), Mwanza, Ruvuma na Tanga (nne kila moja), Iringa, Mara, Geita, Shinyanga na Dar es Salaam (tatu kila moja).

Akitoa maagizo hayo, Waziri Ummy alisema kutokana na wakurugenzi kuwa na wajibu wa kuhakikisha taarifa za hesabu za mwisho zinaandaliwa kwa usahihi, ameshauri mamlaka ya uteuzi wao kuchukua hatua stahiki kadiri itakavyoona inafaa.

Aliagiza ofisi za wakuu wa mikoa na mamlaka za midhamu zihakikishe hatua stahiki zinachukuliwa dhidi ya waweka hazina waliohusika na uandaaji wa taarifa za hesabu za mwisho katika halmashauri hizo.

"Ofisi za wakuu wa mikoa na mamlaka za nidhamu zihakikishe hatua zinachukuliwa kwa wakuu wa vitengo vya ukaguzi wa ndani wa halmashauri 54 ambao hawakukagua taarifa za hesabu za mwisho kabla ya kuziwasilisha kwa CAG,"alisema.

Pia alisema wakuu wa mikoa wahakikishe wanashiriki mikutano maalum ya mabaraza ya madiwani katika halmashauri kujadili taarifa za CAG na kusimamia utekelezaji wa mapendekezo yote pamoja na kuratibu kufanyika kwa uhakiki wa majibu ya hoja zote za ukaguzi na Ofisi yake ipate taarifa za utekelezaji na mpangokazi kabla ya Mei 31, mwaka huu.

"Halmashauri zilizopata hati mbaya na hati zenye shaka ziwabainishe, wataalam wa fedha wenye CPA (T) ambao walisaini (walitia saini) taarifa za hesabu za mwisho kuthibitisha kwamba taarifa hizo ni sahihi na hazina makosa wafikishwe Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA) ili wachukuliwe hatua," alisema.

Waziri huyo alibainisha maelekezo mengine kuwa ni wakurugenzi kuhakikisha wanavijengea uwezo na kuvitumia ipasavyo vitengo vya ukaguzi wa Ndani.

Kuhusu kutorejeshwa kwa mikopo inayotolewa kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, Waziri huyo aliagiza halmashauri kusimamia utekelezaji wa kanuni za utoaji na usimamizi wa mikopo za mwaka 2019 na kuchukua hatua stahiki kwa kikundi kitakachoshindwa kurejesha mkopo.

Pia aliagiza kupitiwa upya mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri kwa lengo la kufanyia kazi dosari zote zilizobainishwa na CAG kuhusu mfumo huo na pia vituo vyote vya kutolea Huduma za Afya vinavyojengwa sasa, vihusishe uwekaji wa mfumo wa kielektroniki wa GoTHOMIS.

Pamoja na hayo, alisema anakusudia kuandaa mikataba ya ufanisi kwa wakuu wa mikoa ili kuongeza uwajibikaji.


bgtl

**BEST GROUP (T) LIMITED**

Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa Idhini tuliyopewa na **NMB BANK** Tunatoa notisi ya siku kumi na nne(14) kuanzia Tarehe ya Tangazo hili kwa mdaiwa aliyetajwa hapo chini, alipe deni analodaiwa na benki hiyo pamoja na riba. Kushindwa kulipa kwa muda huo tutalazimika kuuza dhamana (mali) iliyodhamini mkopo wake kwa **MNADA WA HADHARA**.Mnada utafanyika kuanzia **saa 4:00 Asubuhi** na kuendelea mahali dhamana ilipo kama inavyoonesha hapo chini.

| Na. | JINA LA MDAIWA/MDHAMINI | MAELEZO YA DHAMANA NA MAHALI ILIPO |
|---|---|---|
| 1. | JULIANA INPUT COMPANY/ ATUPAKISYE JOSIAH MWAMGOGWA | Nyumba ya makazi yenye hati Na.164226 kiwanja no.293, kitalu "2" iliyopo Kwembe Manispaa ya Kinondoni kwa jina la Atupakisye Josiah Mwamgogwa. |

**MASHART YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa, au mshindi wa pili atapewa ushindi.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:**
**Mkurugezi Mtendaji**
**Best Group (T) LTD**
**Alli Hassan Mwinyi Road**
**Green Acres Buliding, 2nd Floor.**
**P.O. BOX 1088**
**DAR ES SALAAM**
**MOBILE + 255 715-363537/ +255 765-363537**
**Email: info@bestgoup.co.tz**

**AU**

**Mkurugezi Mtendaji**
**NMB Bank PLC,**
**Ohio Street / Ali Hassan MwinyiRoad,**
**P.O. BOX 9213,**
**DAR ES SALAAM**
**Telephone: +255 22 2322550**
**email: Benedicto.Baragomwa@nmbbank.co.tz**

# ‘Mwekezaji wa bangi’ jela miaka 30

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Moshi imemhukumu mwekezaji wa kigeni, Damian Jankowski na mkewe Eliwaza Pyuza, kutumikia kifungo cha miaka 30 jela kila mmoja, baada ya kuwakuta na hatia katika kesi ya ulimaji wa dawa za kulevya na kufanya mauzo ndani na nje ya Tanzania.

Jana, Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Bernazitha Maziku, wakati anasoma hukumu hiyo, alisema mbali na kifungo hicho, mali zote za mshtakiwa wa kwanza na wa pili, ikiwamo zaidi ya Sh. milioni 26.7 zilizokutwa ndani kwao, shamba lililokuwa limezungushiwa uzio na kulimwa dawa za kulevya aina ya bangi, zinataifishwa na serikali.

Katika kesi hiyo, namba 79 ya mwaka 2020, Hakimu Maziku amewahukumu pia mshtakiwa wa pili, Pyuza, mshtakiwa wa tatu ambaye ni mfanyabiashara, Hanif Kanani na mshtakiwa wa nne, Boniface Kessy, kulipa faini ya Sh. milioni nne kila mmoja au kwenda jela miaka mitatu. Jankowski na Pyuza, mfanyabiashara Hanif Kanani na Boniface Kessy, wanakabiliwa na makosa manne ya kulima bangi ya kisasa miche 729, kujihusisha na matumizi ya bangi, kufanya mauzo na kusafirisha bangi kwenda ng'ambo. Katika hukumu hiyo, Hakimu Maziku alisema: “Mahakama hii ilijiuliza maswali manne ambayo yalipaswa kujibika kabla ya kutoa hukumu. Kama kweli mshtakiwa wa kwanza, wa pili na watatu walikuwa wakilima bangi, kama kweli walikuwa wakijihusisha na kosa la kusafirisha bangi, na kama mshtakiwa wa kwanza, wa pili na wa tatu walikuwa wakitumia dawa hizo za kulevya.

“Kwenye kosa la kusafirisha bangi, ushahidi umekuwa mgumu kuthibitishwa kwa mshtakiwa wa tatu. Na kwenye ‘burden of proof’ kwa mshtakiwa wa kwanza, (uthibitisho wa jinsi gani alizipata) hizo Sh. milioni 26 na zaidi, hakuna taarifa ya kibenki, wala miamala iliyotolewa mahakamani kuthibitisha ni jinsi gani alizipata fedha hizo kihalali.

“Katika kosa la usafirishaji dawa za kulevya, mahakama hii imeona mshtakiwa wa kwanza na wa pili wametenda kosa hilo.”

Februari 17, mwaka huu, mahakama hiyo ilimwona Jankowski na washtakiwa wenzake watatu ambao ni raia wa Tanzania, wana kesi ya kujibu katika mashtaka hayo.

Hakimu Maziku, aliwaona washtakiwa wote wana kesi ya kujibu, baada ya upande wa mashtaka kufunga ushahidi wa mashahidi wa upande wa mashtaka.

Upande wa mashtaka, uliokuwa ukiongozwa na Mawakili wa Serikali kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (NPS), Ignas Mwinuka na Verdiana Mlenza, ulifunga ushahidi wake, baada ya mashahidi 11 kutoa ushahidi wao pamoja na kuwasilisha vielelezo 36.

Katika hati ya mashtaka, washtakiwa hao wanakabiliwa na mashtaka manne ambayo ni kulima dawa za kulevya kinyume na kifungu cha 11 (1) (a) cha Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), Namba 5 ya Mwaka 2015.

Mshtakiwa wa kwanza, pili na wa tatu wote kwa pamoja wanadaiwa kuwa Februari 8, mwaka jana, huko katika eneo la Njia panda ya Himo, Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro, walikutwa wamelima miche ya bangi 729.

Wakati kosa la pili ambalo linawakabili mshtakiwa wa kwanza, pili na wa tatu, ni kusafirisha bangi kinyume cha kifungu cha 15A (1) (2) (C) cha Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Namba 15 ya Mwaka 2017 kama ilivyofanyiwa marejeo.

Kwa mujibu wa hati ya mashtaka, washitakiwa hao pia wanadaiwa kukutwa na kilogramu 15.6 za bangi katika eneo la Shirimatunda, Manispaa ya Moshi, Februari 8, mwaka jana. Kosa la tatu ni kusafirisha dawa za kulevya kinyume na kifungu cha 15A (1) (2) (C) cha Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Namba 5 ya Mwaka 2015 kama ilivyofanyiwa marejeo kifungu cha 9 cha Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Namba 15 ya Mwaka 2017.

Na kosa la nne ni matumizi ya dawa za kulevya, kinyume cha kifungu cha 18 (a) cha Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Namba 5 ya Mwaka 2015.

## Katambi anusa ufisadi ujenzi wa maabara

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MBUNGE wa Shinyanga Mjini, Patrobas Katambi, amepinga Sh. milioni 85.7 kujenga maabara katika Zahanati ya Chibe kwa kuwa kiasi hicho ni kikubwa.

Katambi ambaye pia ni Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu( Kazi, Vijana na Ajira), alibainisha hayo alipofanya ziara kukagua ujenzi wa maabara katika zahanati hiyo ambayo iko kwenye hatua ya msingi ikiwa imeshatumia Sh. milioni 5.7 huku gharama zake hadi kukamilika zikitajwa kuwa ni Sh. milioni 85.7.

Alisema haiwezekani maabara ya zahanati hiyo ikatumia kiasi hicho kikubwa cha fedha wakati jengo la zahanati likitumia Sh. milioni 50.

“Mimi kama Mbunge, sikubaliani na kiasi hiki cha fedha kujenga maabara kwenye zahanati hii. Fedha hizo ni nyingi sana, fanyeni mapitio ili nione namna ya kusaidia kwenye ujenzi huu gharama zake ziwe chini,” alisema Katambi.

Alisema wakati ujenzi wa maabara hiyo ukiendelea, atasaidia upatikanaji wa vifaa na kutengwa chumba maalumu ili wananchi wa eneo hilo watibiwe kwa vipimo na si kwa dalili za ugonjwa kama inavyofanyika hivi sasa.

Katika hatua nyingine, Katambi alitoa Sh. 200,000 kwa ajili ya kufungwa mfumo wa umeme (wiring) kwenye zahanati hiyo ili ipate umeme na kutoa huduma stahiki kwa wananchi sehemu yenye mwanga na siyo kutumia mwanga wa tochi za simu.

Naye Meya wa Manispaa ya Shinyanga, David Nkulila, aliunga mkono maoni ya mbunge huyo kwa kupinga fedha nyingi kujenga maabara hiyo.



Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Ally Hapi (mwenye barakashia), akikagua ujenzi wa barabara ya Ngosha - St. Dominic-Ngelewala- Kihodombi, ambayo inahudumia wakazi wa Mwangata na Isakalilo katika Manispaa ya Iringa na kusimamiwa na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), wakati wa ziara yake ya kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo jana. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

# Matukio ya mauaji wivu wa mapenzi yaongezeka

**Na Christina Mwakangale**

RIPOTI ya Haki za Binadamu ya mwaka 2020 iliyotolewa na Kituo Cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) imeeleza kuwa matukio ya mauaji yatokanayo na wivu wa mapenzi yameongezeka kutoka 12 mwaka 2019 hadi 23 mwaka jana.

Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Anna Henga, alisema mienendo ya hivi karibuni inaonyesha kwamba matukio ya wanawake kuuawa na wenza wao, yameongezeka kutokana na wivu wa mapenzi.

Henga alisema LHRC ilibaini kuwa mauji hayo baadhi hufanywa na wenza wanaoishi pamoja au wenza walioachana.

“Kwa mwaka 2019, LHRC ilikusanya matukio 12 ya mauaji ya wanawake yaliyofanywa na wenza wao, huku matukio manane yakihusishwa na wivu wa kimapenzi.

“Mwaka 2020, LHRC ilikusanya matukio 32 ya mauaji ya wanawake yaliyofanywa na wenza wao, matukio 23 yalisababishwa na wivu wa mapenzi. Mauaji haya ni ukatili dhidi ya wanawake na yanakiuka uhuru wao dhidi ya ukatili pamoja na haki ya kuishi,” alisema Henga na kuongeza;

“Matukio hayo ni zaidi ya mara mbili yaliyotokea mwaka 2020, ikilinganishwa yaliyoripotiwa mwaka 2019.”

Alisema haki tano kati ya zilizofanyiwa utafiti ilibainika kukiukwa zaidi ikiwamo haki ya kuishi ambayo yalihusisha mauaji yaliyotokana na watu kujichukulia sheria mkononi, imani za kishirikina na kijinsia.

Alisema haki nyingine iliyokiukwa ni haki ya uhuru wa kujieleza, utungaji na marekebisho ya utekelezaji wa sheria na ukatili wa kingono na kimwili dhidi ya wanawake, watoto na wazee.

“Ukamataji na uwekaji kizuizini watu kinyume na sheria, uchunguzi kuchelewa kukamilika, kutotoa dhamana, ubambikaji wa kesi, kukosa uhuru wa kujumuika ni kati ya haki zilizokiukwa,” alisema Henga.

Aidha ripoti hiyo ilisema kutoandaliwa kwa wosia mapema, ni kati ya sababu za chanzo cha migogoro ya ardhi huku wanawake na watoto wakiathiriwa zaidi.

“Watanzania wengi bado wana hofu ya kuandaa wosia, wakidhani wanajichulia kifo, matukio na matatizo mengi ambayo LHRC tunakutana nayo ni pamoja na masuala ya umiliki wa ardhi,” alisema Henga.

Kadhalika, ripoti ilionyesha kulikuwa na mauaji ya watu 122 yaliyotokana na imani za kishirikina pamoja na upungufu wa asilimia 42 wa watumishi katika mhimili wa Mahakama.

Alisema kama ilivyokuwa kwa mwaka 2019, idadi ya ajali za barabarani na vifo vimepungua kwa mwaka jana, kutokana na juhudi za Jeshi la Polisi na wadau.

Ripoti ilieleza kwamba ajali 10,297 zilizotokea mwaka 2016 zilipungua na kufikia 2,924 mwaka 2019, sawa na punguzo la asilimia 56 huku mwaka jana ziliripotiwa ajali 1,714 na vifo ni 1,260.

# Uchunguzi kifo cha mwandishi wa ITV waendelea

**Na Christina Mwakangale**

JESHI la Polisi Mkoa wa Kinondoni, limesema bado linaendelea na uchunguzi kuwabaini waliohusika na mauaji ya aliyekuwa mwandishi wa habari wa ITV/Radio One, Blandina Sembu.

Kamanda wa Polisi mkoa huo, Ramadhani Kingai, aliiambia Nipashe jana, alipoulizwa kuhusiana na hatua zilizofikiwa katika uchunguzi wa suala hilo.

Blandina ambaye pia alikuwa mtayarishaji wa kipindi cha Jarida la Wanawake ITV, alifariki dunia Machi 27, mwaka huu, baada ya mwili wake kuokotwa eneo la Bamaga-ITV, Mwenge, Dar es Salaam.

Baada ya tukio hilo, Jeshi la Polisi lilisema Blandina alifariki dunia baada kupigwa na kitu chenye ncha kali usoni.

Kamanda Kingai alisema mwili wa Blandina uliokotwa eneo la Maryland Bar, njia panda ya ITV na watu wasiofahamika wakiwa na gari aina ya Toyota Noah, ambalo halikutambuliwa namba zake za usajili.

"Walisimamisha gari eneo hilo, kwa muda mfupi na lilipoondoka ulipatikana mwili wa jinsia ya kike na baadaye alitambulika kuwa ni Blandina Sembu (47), mfanyakazi wa ITV/ Radio One," alisema Kamanda Kingai.

"Eneo alikookotwa ni Area B, alikouliwa ni kwingine sababu mwili ulionekana muda mfupi tu eneo la Bamaga, hivyo uchunguzi unaendelea," aliongeza.

Kamanda huyo alisema Sembu alikuwa mkazi wa Zinga, Bagamoyo mkoani Pwani.

Mwili wa Blandina uliagwa Dar es Salaam, Machi 31, mwaka huu, kisha kusafirishwa kwa maziko Musoma mkoani Mara.



Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mhandisi, Hamad Yussuf Masauni, akijibu swali la Mbunge wa Jangómbe, Ali Hassan Omar King, kuhusu wajibu wa kumlipa mteja aliyeibiwa fedha kwenye akaunti ya benki, bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: WFM**

# Serikali kufuatilia uchunguzi wizi mil. 400/- za wateja NBC

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Fedha na Mipango imeahidi kufuatilia uchunguzi wa madai ya wateja 103 wa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) Tawi la Forodhani, Zanzibar, kuibiwa zaidi ya Sh. milioni 400 na watumishi wasio waaminifu wa benki hiyo.

Ahadi hiyo ilitolewa jana baada ya Mbunge wa Jang'ombe (CCM), Ali Hassan Omar King, kuliza swali la nyongeza bungeni na kuhoji lini wateja hao watalipwa fedha zao na kuichukulia hatua benki hiyo kwa kutowalipa.

Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Hamad Yusuph Masauni, alisema atafuatilia wizi huo ili kujua kama uchunguzi wa jambo hilo umefanyika na nani aliyesababisha uhalifu huo.

Alisema kama linasababishwa na mfumo wa kibenki basi Benki Kuu ya Tanzania (BoT) itachukua dhamana kuhakikisha fedha hizo zinarudishwa na benki husika.

Katika swali la msingi, Mbunge huyo alihoji wizi unapotokea kwenye akaunti ya benki ya mteja uliofanywa na mtumishi wa benki, ni nani mwenye wajibu wa kumlipa mteja.

Naibu Waziri Masauni alisema wizi unapotokea, uchunguzi wa kina hufanywa na vyombo husika katika masuala ya upelelezi ikiwa ni pamoja na Jeshi la Polisi na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kwa kadri hali na mazingira ya tukio yatakavyokuwa.

"Endapo itabainika kuwa wizi huo umefanywa na mtumishi wa benki, hatua stahiki huchukuliwa kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo ikiwa ni pamoja na mteja kulipwa kiasi alichoibiwa na mhalifu kuchukuliwa hatua za kinidhamu pamoja na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria," alisema.

Pia alisema BoT hutoa adhabu kwa benki husika pale inapobainika utaratibu uliowekwa na benki husika ulikuwa na kasoro zilizochangia kuibiwa kwa fedha za mteja.

# Watumishi halmashauri wadaiwa kusababisha upotevu wa mil. 45/-

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

WATUMISHI watatu wa Idara ya Biashara katika Halmashauri ya Mji Masasi mkoani Mtwara na vibarua wanane, wanadaiwa kusababisha upotevu wa Sh. milioni 45.

Hatua hiyo inadaiwa kuwa imeisababishia halmashauri hiyo kukosa mapato ya ndani yatokanayo na ushuru.

Kutokana na hali hiyo, Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Mji wa Masasi linajipanga kuchukua hatua dhidi ya watumishi hao.

Hayo yalisemwa jana na Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Hashim Namtumba, alipokuwa akizungumza na Nipashe kuhusu madai hayo.

Alisema madai hayo ni kweli na kwamba suala hilo lilishafikishwa mbele ya madiwani wa halmashauri katika kikao kilichofayika Febuari, mwaka huu.

Namtumba alisema watumishi hao walielezwa kurejesha fedha zote zinazodaiwa kupotea na kwamba licha agizo hilo, kikao cha baraza la madiwani kitakachofanyika mwishoni mwa mwezi huu, kitakuja na adhabu dhidi yao.

Alisema watumishi ambao wamehusika na upotevu wa fedha hizo watatu ni kutoka Idara ya Biashara ya halmashauri. Alisema fedha hizo zilikuwa zikikusanywa kupitia mashine za kieletroniki za kukusanyia ushuru kwenye maeneo mbalimbali ya biashara.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, ndani ya halmashauri hiyo kumekuwa na tatizo kubwa la ukosefu wa nidhamu katika kukusanya mapato ya ndani kwa baadhi ya watumishi.

"Upotevu wa fedha hizi ulibainika baada kupitia taarifa iliyotolewa na kamati ya fedha katika kikao cha baraza la madiwani mapema mwaka huu na wajumbe hawakufurahishwa na jambo hili," alisema Namtumba.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Masasi, Gimbana Ntavyo, alisema madai hayo ni kweli na kwamba watumishi hao 11 walishapewa muda wa kuanza kuzilipa fedha hizo kidogo kidogo.

"Ni kweli wako watumishi ambao wamesababisha upotevu wa fedha za mapato ya ndani ya halmashauri kiasi cha Sh. milioni 45. Fedha hizi wamezipoteza kupitia mfumo wa fedha," alisema Ntavyo.

Alisema tatizo hilo limetokana na mifumo ya kifedha kupitia mashine za kieletroniki ambazo zilikuwa zikitumiwa na watumishi hao kukusanya ushuru.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Utulivu, umakini muhimu kuelekea lala salama Bara

**ZIKIWA** zimebakia raundi tisa ili kumalizika kwa msimu wa mwaka 2020/21 wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo inashirikisha timu 18 za hapa nchini, mambo mbalimbali ya kuzingatia yanahitajika ili kuhakikisha msimu husika unamalizika vizuri.

Ligi Kuu Bara ndio ligi ya juu kwa upande wa Tanzania Bara ambayo hutoa mwakilishi wa mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, wakati bingwa wa michuano ya Kombe la Shirikisho hupata nafasi ya kwenda kupeperusha bendera ya nchi katika Kombe la Shirikisho Afrika.

Kuelekea hatua ya lala salama, klabu zinatakiwa kutumia muda wake mwingi katika kuimarisha vikosi vyake kwa lengo la kusaka matokeo chanya wanaposhuka dimbani na si kufanya mambo mengine ambayo yanaweza kuwapoteza.

Inafahamika wapi timu iliyoandaliwa vyema au wachezaji waliopitia misingi inayostahili ndio wenye nafasi ya kuzalisha matokeo chanya na si jambo lingine lolote nje ya hapo.

Nipashe inazikumbusha timu zote zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara kuhakikisha zinaendelea kuchanga vyema karata zake na hatimaye kufikia malengo waliyojiwekea kwa sababu muda wa kujiimarisha bado upo.

Mechi tisa kwa timu ambazo hazina viporo zinaweza kubadilisha nafasi uliopo katika msimamo na hatimaye kumaliza msimu kwa kicheko kwa timu ambayo itafanikiwa kutwaa ubingwa lakini pia kwa wale ambao watanusurika na janga la kushuka daraja ambalo hakuna timu inayopenda kulishuhudia.

Kama nafasi ya kutwaa ubingwa bado iko wazi, ni vyema kwa klabu zote kuendelea kupambana kuhakikisha wanaondoka na ushindi wanapoingia uwanjani kwa sababu huwezi kujua Mungu amewaandalia zawadi gani kutokana na jitihada walizozionyesha wakati wote wa msimu.

Vile vile katika upande wa timu zinazoburuza mkia, kwa idadi ya mechi zilizosalia hakuna klabu ambaye imejihakikishia kujinasua kwenye janga hilo kwa sababu katika soka lolote linaweza kutokea na 'bundi' akahamia kwenye klabu yako.

Tunawakumbusha huu si wakati wa kupoteza katika kuendesha michakato ya nje ya uwanja kwa sababu haitasaidia timu kuvuna pointi za uwanjani na matokeo yake mtawakosesha mashabiki wetu furaha ya kushuhudia michezo ya Ligi Kuu pale timu hizo zinapokuwa kwenye viwanja vya nyumbani.

Vita ya kushuka daraja inawezekana ikaonekana ni vita nyepesi, lakini vile vile ni vita yenye ushindani mkubwa kwa sababu timu zilizoko mkiani zinatofautiana kwa pointi chache hivyo kikosi kinachofanikiwa kupata ushindi wa mechi moja, mbili au sare, hupaa kwa nafasi zaidi ya moja na kurejesha matumaini ya kusalia kwa ajili ya msimu ujao.

Ingawa tunawakumbusha ni makosa kukata tamaa kabla ya filimbi ya mwisho ya halijapulizwa, lakini dalili za 'kuzama' au kuibuka mfalme wa msimu huanza kuonekana wakati hatua ya lala salama ikianza kukaribia. Hata hivyo baadhi ya timu zinatakiwa zibadilishe mwenendo wake kwa sababu kila msimu zinaonekana kutoonyesha ushindani wowote wa kuwania ubingwa na badala yake wamekuwa wasindikizaji kwa kuridhika pale wanapobaini wako kwenye nafasi salama.


Mbali na Ligi Kuu Tanzania Bara, bado kuna nafasi ya kujirekebisha kwa timu ambazo zimesalia katika mashindano ya Kombe la FA ambayo bingwa wake naye hukata tiketi ya kushiriki michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Kupanga ni kuchagua, timu inayohakikisha inaendelea kupanga vyema hesabu za kusaka ushindi uwanjani zitafanikiwa na wale ambao watatumia muda wao katika masuala ya 'porojo', watajichimbia kaburi wenyewe. Nidhamu na utulivu ndio silaha muhimu inayohitajika katika kipindi hiki ili kila timu itimize malengo chanya iliyojiwekea na hatimaye kuanza maandalizi ya msimu mpya kwa weledi.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com


## Muungwana Lazima Nilonge



Na Barnabas Maro

# Ndugu m-baya humshinda...

**TAIB!** (Tamko la kuafiki jambo linalosemwa; bila shaka.) Ndugu m-baya humshinda rafiki mzuri. Maana yake hata rafiki akawa mzuri kiasi gani hawezi kuwa sawa na ndugu yako hata akawa m-baya.

Methali hii hutumiwa kutukumbusha umuhimu wa kuwathamini ndugu zetu au watu tulio na ujamaa nao kwa kuwa wanaweza kutufaa kuliko wanavyoweza kufanya marafiki zetu.

Simba na Yanga ni timu za nchi moja iitwayo Tanzania, tena jiji moja ambalo zamani liliitwa Bandari ya Salama na sasa inaitwa Dar es Salaam. Sioni ni kwa nini baadhi ya wanachama na mashabiki wao watakiane na kuwekeana shonde, yaani hali ya watu kutosemezana kutokana na ugomvi wao wa zamani; mfundo, chuki, uhasidi.

Zamani timu hizo zilikuwa moja lakini mwaka mmoja baadaye zilitofautiana na kutengana. Tangu wakati ule zimekaliana vibaya kila moja ikiichukia nyingine ! Kwa nini? Ndo maana wahenga walisema : " Chuki humchoma anayeihifadhi." Twafunzwa umuhimu wa kutoiweka chuki kwa kuwa tunajidhuru wenyewe.

Tunaambiwa jogoo wawili hawawezi kusaidiana kukikamata kidudu. Maana yake jogoo wawili hawawezi kupatana na kusaidiana kukikamata kidudu kidogo. Methali hii yatufahamisha kuwa watu wanaoshindana hawawezi kushirikiana kufanya jambo hata kama ni dogo sana!

Upendo kwa watu wote hata adui. "Wabarikini wanaowaudhi; lieni pamoja na waliao. Msimlipe mtu ovu kwa ovu. Angalieni yalio mema machoni kwa watu wote.

Timu ya Simba ipo Dar es Salaam, Tanzania kama ilivyo Yanga. Mwaka huu kuna matumaini makubwa Simba kutwaa ubingwa wa Afrika na kuwa timu ya kwanza hapa nchini na ukanda wa Afrika Mashariki kutwaa taji hilo. Tunapaswa kuiombea Mungu na kuishangilia kwa hoihoi, yaani sauti ya furaha, shangwe na nderemo; chereko, vifijo.

> **Kama nafasi ya kutwaa ubingwa bado iko wazi, ni vyema kwa klabu zote kuendelea kupambana kuhakikisha wanaondoka na ushindi wanapoingia uwanjani kwa sababu huwezi kujua Mungu amewaandalia zawadi gani kutokana na jitihada walizozionyesha wakati wote wa msimu.**

Wakati timu hiyo inapoelekea kukamilisha michezo yake inayowakutanisha mabingwa wa Bara la Afrika msimu huu tuweke tofauti zetu kando na kuiombea Simba kwa Muumba wetu aisaidie ili iwe timu ya kwanza sio Tanzania tu bali Afrika ya Mashariki, kutwaa kombe la Mabingwa wa Afrika lililotwaliwa mara nyingi na timu za Uarabuni, hasa Al Ahly ya Misri.

Itakapokuwa hivyo, Tanzania itaogopwa na timu zingine za Bara la Afrika na kuheshimiwa badala ya kulinganishwa na 'jamvi la wageni' kwa miaka kadhaa. Kwa hiyo Simba itakapotwaa kombe hilo, Tanzania itatambulika sio Afrika tu, bali hata Ulaya, Marekani na kwingineko duniani.

Halahala wana Yanga wenzangu wanaoiombea vibaya Simba wakati huu inapokaribia kuwa Bingwa wa Kandanda Barani Afrika waache tabia hiyo, vinginevyo tutachekwa na kudharauliwa sana na hao tunaowashangilia.

Timu yoyote ya Tanzania inapofanya vizuri na timu za ughaibuni twapaswa kuweka kando tofauti zetu. Kinachoshangaza ni kwamba Simba na Yanga ndizo zinazofanyiana ubaya mojawapo inapocheza na timu ya ughaibuni ili ishindwe!

Mojawapo inapocheza na timu ngeni na kuizombea timu ya nyumbani, hasa inaposhindwa tunajifadhaisha wenyewe. Ebo! ndugu yetu anapigwa na mgeni kisha twashangilia na kumzomea ndugu yetu? Pukachaka!

Twaambiwa "Kilichompata ngwena (mamba) na kiboko ni chicho." Maana yake hatari inayoweza kumfika mamba lazima itamfika kiboko kwani wanaishi katika mazingira mamoja.

Methali hii hutumiwa katika mazingira ambapo jambo fulani baya limpatapo mtu fulani linaishia kumpata au kumfika mwenzake.


**marobarnabas@yahoo.com**
**0784-334 096**

HABARI BUNGENI



Mbunge wa Bahi, Keneth Nollo, akichangia mada Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA IBRAHIM JOSEPH**

# Ajira mpya 6,000 walimu sasa Juni

SERIKALI imesema itaajiri walimu wapya 6,000 wa shule za msingi na sekondari ifikapo Juni, mwaka huu, ili kujaza nafasi zilizoachwa na walimu waliofariki au kustaafu kazi.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, alibainisha hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Njombe Mjini (CCM), Deodatus Mwanyika.

Katika swali lake, Mbunge huyo alimshukuru Rais kwa kutoa ajira za walimu 6,000 ili kujaza nafasi wazi huku akieleza kuwa licha ya kufanya hivyo bado mahitaji ni makubwa hususani uamuzi wa serikali kutoa elimu bure.

"Napenda kujua je, serikali inaweza kutoa 'comitment' ya kuajiri walimu wa kutosha sababu namba iliyotajwa bado ni ndogo?" alihoji.

Katika swali lingine, alisema ugawaji walimu katika maeneo mbalimbali kuna vigezo lakini maeneo ya halmashauri na miji vinavyotumika havina uhalisia maana yanaangaliwa sababu yana miji wakati yapo maeneo ya vijijini hakuna shule.

Kutokana na hali hiyo, alihoji kama wizara itakuwa tayari kupitia upya vigezo ili maeneo yenye kilomita zaidi ya 25 yapate walimu ili elimu iwe na tija.

Akijibu maswali hayo, Silinde alikiri kwamba alichokisema mbunge kuwa bado kuna tatizo la walimu huku akisema serikali itaendelea kuajiri kadiri ya upatikanaji wa fedha na imejipanga kuhakikisha inaondoa kabisa tatizo hilo.

Kuhusu vigezo, alisema wamepokea ushauri huo na kwamba watauzingatia ili kuhakikisha ugawaji walimu katika maeneo mbalimbali unafuata usawa na kwa haki nchi nzima.

Katika swali la msingi, Mwanyika alihoji serikali inachukua hatua gani kumaliza upungufu wa walimu nchini hasa shule zilizoko maeneo ya vijijini.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Silinde alisema ili kukabiliana na uhaba wa walimu katika shule za msingi na sekondari, kuanzia Desemba 2015 hadi Septemba 2020, serikali imeajiri walimu 10,666 wa shule za msingi na walimu 7,515 wa shule za sekondari na kuwapanga kwenye maeneo yenye uhitaji mkubwa.

Aidha, alisema kuanzia Desemba 2015 hadi Septemba 2020, Halmashauri ya Mji Njombe imeajiri walimu 21 wa shule za msingi na walimu 111 wa shule za sekondari.




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA

## Mbunge ataka mfumo wa kidijitali zahanati

MBUNGE wa Bahi (CCM), Kenneth Nollo, ameitaka serikali kuanzisha mfumo wa kieletroniki wa uendeshaji wa huduma za afya (GoTHOMIS) kwenye zahanati kama ilivyo kwenye vituo vya afya ili kuondoa mwanya wa upotevu wa mapato.

Akiuliza swali bungeni jana, Nollo alihoji mpango wa serikali wa kuanzisha mfumo huo.

Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange, alisema mfumo huo ni wa kukusanya taarifa za afya kwa wagonjwa ikiwa ni pamoja na taarifa za malipo ya matibabu na huduma za afya.

"Mfumo umeunganishwa na mfumo wa kielekroniki wa ukusanyaji wa mapato ya serikali (GePG), hivyo kuwezesha wapewa huduma kulipa moja kwa moja benki au kupitia mitandao ya simu na kuwezesha makusanyo ya kituo kwenda moja kwa moja kwenye akaunti za kituo cha kutolea huduma za afya," alisema.

Aidha, alisema hadi Februari, mwaka huu, mfumo wa GoTHOMIS umesimikwa katika hospitali 21 za mikoa, hospitali 82 za halmashauri, hospitali teule za wilaya 22, vituo vya afya 385 na zahanati 411.

"Kazi ya kusimika mfumo huu katika vituo vya kutolea huduma za afya katika ngazi zote nchini inaendelea," alisema.

Alisema halmashauri zimekuwa zikitumia vyanzo vyake vya ndani kusimika mtandao kiwambo (LAN) na kununua vifaa vingine zikiwamo kompyuta kisha wataalam wa halmashauri husika kwa kushirikiana na wataalam wa teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) ngazi za mikoa kuusimika mfumo na kutoa mafunzo kwa watumiaji wa mfumo.

# Uwekezaji wa viwanda kupunguza gharama uagizaji dawa, vifaa tiba

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inaendelea kufuatilia wawekezaji 11 wanaoendelea na ujenzi wa viwanda vya dawa na vifaa tiba ili kuokoa fedha ambazo zinatumika kuagiza kutoka nje ya nchi.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, aliyasema hayo bungeni wakati akijibu swali la Mbunge wa Singida Mjini(CCM), Mussa Sima.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji serikali imeweka mkakati gani wa kuanzisha viwanda vya dawa na vifaa tiba nchini ili kuachana na kuagiza dawa na vifaa tiba hivyo nje ya nchi.

Akijibu swali hilo, Kigahe alisema ujenzi umefikia hatua mbalimbali na lengo la serikali ni kuokoa fedha ambazo zinatumika kuagiza dawa na vifaa tiba hivyo kutoka nje ya nchi.

Alisema hatua hiyo itasaidia upatikanaji wa uhakika wa dawa hizo nchini, hivyo kuendelea kutengeneza ajira nchini na kwamba lengo la kufanya hivyo ni kuhakikisha afya za Watanzania zinakuwa suala la kipaumbele wakati wote.

"Sekta ya viwanda katika dawa na vifaa tiba ina viwanda 14 ambapo viwanda 12 vinatengeneza dawa za binadamu, viwili dawa za mifugo na kiwanda kimoja kinatengeneza vifaa tiba. "Wizara imeendelea kuchukua hatua za makusudi ili kuhakikisha sekta hiyo inaongeza uwekezaji kwenye viwanda vya dawa na vifaa tiba," alisema.

Hatua hiyo, alisema inakwenda sambamba na kuongeza ufanisi wa viwanda vilivyopo ili kufikia asilimia 60 ya uwezo wa uzalishaji wa dawa na vifaa tiba nchini ifikapo mwaka 2025.

Alizitaja hatua hizo kuwa ni pamoja na kuunda Kamati ya Kitaifa inayoshughulikia Sekta ya Viwanda vya Dawa na Vifaa Tiba (NPCC) na kuweka vivutio vya uwekezaji kwa lengo la kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

"Ili kuvutia wawekezaji katika sekta hiyo, serikali imeondoa VAT (kodi ya ongezeko la thamani) kwenye vifungashio vya dawa zinazozalishwa nje na ndani ya nchi. Pia imeshusha kodi ya mapato kwa asilimia 30 ambayo imesaidia kuhamasisha uwekezaji mpya na upanuzi wa viwanda, kwa muda wa miaka miwili kwa miradi mipya ya viwanda vya dawa na kuweka upendeleo maalum kwa ununuzi wa dawa zinazozalishwa na viwanda vya ndani kupitia Bohari Kuu ya Dawa (MSD).

Katika swali la nyongeza, Mbunge huyo alisema kuwa licha ya jitihada zilizopo bado serikali inaagiza dawa na vifaa tiba kwa asilimia 80 nje ya nchi na kuhoji hali hiyo inatokana na ushindani wa kibiashara au vipi.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri alisema nchi haijajitosheleza kwa viwanda vya kuzalisha dawa na vifaa tiba na kwamba suala sio ubora bali uwezo haujakidhi mahitaji ya ndani, ndio maana wanahamasisha ili wawekezaji waje kuwekeza.

## Wavuvi wafariki wakivua ziwani

**Na Ahmed Makongo,** BUNDA

WAVUVI wanne wamekufa maji na wengine watatu kunusurika kifo baada ya mtumbwi waliokuwamo kupigwa dhoruba na kuzama wakati wakivua samaki katika Ziwa Victoria, Bunda mkoani Mara.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mara, Kamishna Msaidizi (ACP), Daniel Shilla, alithibitisha juzi kuwa tukio hilo lililotokea majira ya saa mbili usiku Aprili 7, mwaka huu.

Kamanda Shilla alisema: "Tayari nimepatiwa taarifa hiyo kwamba kuna wavuvi wanne wamekufa maji usiku katika Ziwa Victoria wakati wakivua samaki".

Diwani wa Kata ya Neruma, Michael Maungo, na Kaimu Ofisa Mtendaji wa Kata hiyo, Shinji Shinji, waliwataja wavuvi waliofariki katika tukio hilo kuwa ni Kennedy Lukundo (25) mkazi wa kijiji cha Mwiluluma, Geoffrey Mazigo (19) mkazi wa kijiji cha Kisorya, Zacharia Ruhumbika (17) na Masalu Mafuru (22) wote wakazi wa kijiji cha Kenkombyo wilayani Bunda.

Diwani Maungo alisema katika mtumbwi huo kulikuwa na wavuvi saba na kwamba watatu kati yao walinusurika kifo baada ya kuogelea hadi nchi kavu na kutoa taarifa juu ya tukio hilo.

"Tuna msiba mkubwa katika Kata yetu ya Neruma, tumepoteza vijana wetu wanne na katika mtumbwi huo kulikuwa na watu saba, watatu baada ya mtumbwi kupinduka na kuzama waliogelea hadi nchi kavu na ndipo wakatoa taarifa juu ya tukio hilo," alisema Maungo.

Kadhalika, viongozi wa Kata ya Neruma walisema baada ya tukio hilo wananchi walifanya jitihada za kuopoa miili ya wavuvi waliopoteza maisha katika tukio hilo na kwamba tayari miili yote ya watu watatu iliopolewa na kufanyiwa maziko.

Hili ni tukio la pili kutokea wilayani Bunda kwa kipindi kisichozidi miaka miwili, kwani mwaka jana wavuvi wengine wanne walikufa maji wakati wakivua samaki katika ziwa hilo.

# Msako vifungashio vya plastiki waanza

**Na Joseph Mwendapole**

BARAZA la Taifa la Hiofadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), jana lilianza msako dhidi ya watu wanaotumia vifungashio visivyokubalika kisheria.

Sambamba na kuanzisha msako huo, baraza limewataka wafanyabiashara kutii sheria bila shuruti.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alibainisha hayo juzi ana wakati wa mkutano wa pamoja ulioandaliwa na Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania (CTI) na wadau mbalimbali wanaotengeneza vifungashio.

Alisema NEMC imefurahishwa na taarifa kuwa viwanda vya ndani vina uwezo mkubwa wa kuzalisha vifungashio vinavyokidhi matakwa ya kisheria, hivyo hakutakuwa na kisingizio chochote.

"Awali tulikuwa na wasiwasi kwamba je, tutakuwa na vifungashio vipya vya kutosha? Lakini nimehakikishiwa na CTI na wazalishaji wenyewe kwamba vipo vya kutosha. Si nia ya serikali kukamata mtu na kumtoza faini ila tunaomba sheria ifuatwe tusifike huko," alisema Dk. Gwamaka.

Alisema serikali ilitoa muda wa kutosha kwa viwanda kutengeneza vifungashio ambavyo vinafaa kurejelezwa ili baada ya kutumika vikusanywe na vitumike tena kuzalisha hali itakayosaidia kupunguza madhara yatokanayo na bidhaa za plastiki tofauti na sasa.

Alisema NEMC itaendelea kulinda viwanda vya ndani vinavyotengeneza bidhaa hizo kwa kuhakikisha inadhibiti bidhaa zinazotoka nchi jirani ambazo huwa zinapita njia za panya bila kulipa kodi, hivyo kutawala soko la ndani.

Kemilembe Mutasa kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, alisema serikali inashukuru kuona kwamba kuna viwanda hapa nchini ambavyo vitakuwa vinarejeleza mifuko hiyo mipya hivyo kupunguza athari kwa mazingira.

"Tumeenda maeneo mbalimbali kwenye masoko ya Mkoa wa Dodoma tumekuta kuna vifungashio vipya vinavyokidhi matakwa ya kisheria vya kutosha, hivyo tuna uhakika jambo hili litafanikiwa kwa kiwango kikubwa. Changamoto ni kuhakikisha vikishatumika vinarejelezwa ili kuokoa mazingira," alisema Mutasa.

Hussein Sufian kutoka CTI, alisema serikali ilishatoa taarifa kwa umma kuhusu ukomo wa vifungashio visivyotakiwa na NEMC kwa kushirikiana na wadau wengine kama Shirika la Viwango (TBS) wamekaa vikao vingi lengo likiwa ni kuhamasisha umma kufahamu umuhimu wa kutekeleza sheria hiyo. Alisema CTI ambaye ni msimamizi wa wazalishaji wameshaanza kutekeleza agizo la serikali kuhusu vifungashio hivyo na tayari wanachama wake wameshatengeneza vifungashio hivyo vipya vitakavyotumika kuanzia leo.



Mkazi wa Goba, akichota maji kwaajili ya matumizi ya nyumbani kwenye Mto Tegeta, Manispaa Ubungo, mkoani Dar es Salaam mapema wiki hii kutokana na eneo hilo kukosa huduma za maji safi ya bomba. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mkuranga kicheko mradi wa maji kukamilika

**Na Frank Monyo**

WANANCHI wa Wilaya ya Mkuranga wameanza kunufaika na mradi mkubwa wa maji uliogharimu Sh. bilioni 5.6.

Mradi huo umetekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kwa kutumia fedha zake za ndani, ukiwa na lengo la kuondoa adha ya maji ya muda mrefu kwa wakazi wa eneo hilo.

Akizungumza kukamilika kwa mradi huo, Mhandisi wa DAWASA, Richard Katwiga, alisema tayari maji yameshaingia kwenye tangi lenye ujazo wa lita 1.5, mafundi wameshafungulia maji ili kusafisha mabomba kabla ya kupeleka huduma kwa wateja.

"Kuanzia Aprili 2, mwaka huu tumeshaingiza maji kwenye tangi lenye ujazo wa lita 1.5 na leo (juzi) mafundi watafungulia ili kuweza kuyaruhusu maji kusafisha mtandao wa mabomba waliyoyalaza kabla ya kuanza kupeleka huduma kwa wateja,"alisema Mhandisi Katwiga.

Aliongeza: "Zoezi lililobaki ni kuanza maunganisho mapya kwa wateja walioomba kupatiwa huduma ya maji safi".

Mhandisi Katwiga alisema tayari wamelaza mtandao wa mabomba takribani Kilometa 65 katika Kata ya Mkuranga na Kiparang'anda, kwamba wananchi wa maeneo hayo wataanza kufaidika na mradi huo kwenye awamu ya kwanza kabla ya kwenda maeneo mengine ya karibu.

Alisema wapo wananchi walioathirika wakati wa ujenzi wa mradi wa Mkuranga lakini kufikia Oktoba 2019 walianza kupata huduma ya maji kupitia mtandao mpya wa mabomba waliyoyalaza kwa kutumia tangi la zamani lililojenga mwaka 2002.

Aliongeza kuwa kuanzia sasa wanatarajia kufanya maunganisho ya tangi kubwa la maji kwenye mtandao mpya ili wananchi waendelee kupata huduma na kuanza kufanya maunganisho mapya kwa wateja waliofanya maombi.

Mhandisi Katwiga alisema: "Kuna wateja 50 wameshaomba kuunganishiwa huduma ya maji, tutaanza kuwatembelea ili kuwaunganishia huduma ya maji na zaidi lengo la DAWASA ni kuwafikia wananchi wengi zaidi ndani ya mji wa Mkuranga".



# BAKWATA kufanya dua kumuombea Rais Samia

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BARAZA Kuu la Waislamu (BAKWATA) Wilaya ya Dodoma mjini limepanga kufanya dua itakayoongozwa na Sheikh wa Mkoa wa Dodoma, Mustapha Rajabu, kwa ajili ya kumuombea Rais Samia Suluhu Hassan, pamoja na wasaidizi wake ili kutenda haki kwa Watanzania wote bila kujali itikadi.

Mwenyekiti wa Baraza hilo, Bashiru Omary, alibainisha hayo jana jijini Dodoma wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema kuwa, BAKWATA Wilaya ya Dodoma Mjini wanaimani kubwa na Rais Samia Suluhu Hassan kuwa ataongoza kwa kuzingatia misingi iliyopo.

"Tunaimani kubwa sana na Rais na niwaombe Watanzania wote tumuonge mkono katika utendaji wake yeye pamoja na wasaidizi wake,"alisema Sheikh Omary.

Aidha, alisema kuwa lengo la kufanya dua hiyo ni kumuombea kwa Mungu amlinde na kumuongoza katika kutoa uamuzi wenye maslahi na taifa.

Alisema, Rais Samia amekuwa katika uongozi wa juu katika taifa kwa muda, hivyo BAKWATA wanayoimani kuwa atafanya makubwa kwa Watanzania.

"Naomba niwatoe hofu wanaodhani kuwa Rais Samia hataweza kuongoza, naomba waondoe hofu hiyo, na tummpe ushirikano kwani kwa kipindi kifupi ameweza kuonyesha ni kiongozi wa namna gani kupitia hotuba zake,"alisema Sheikh Omary.

Pia, alimshauri Rais kufuata nyayo za mtangulizi wake katika kuwatumikia viongozi wa dini kwenye matukio mbalimbali ya kitaifa ili kuendelea kuiombea nchi kuwa na amani. Pamoja na hayo, pia Mwenyekiti huyo alimpongeza Mufti wa Tanzania Sheikh, Abubakar Zuberi kwa uteuzi wa viongozi wa dini alioufanya hivi karibu.

"Tunampongeza Mufti kwa kazi hii na hawa walioteuliwa tunaomba sasa washirikiane na serikali ili kuhakikisha kuwa nchi inasonga mbele katika kukua kiuchumi,"alisema Sheikh Omary.

Aliwataka walioteuliwa kuhakikisha wanafanya kazi na kuendelea kuhubiri amani katika taifa ili kuondokana na migogoro isiyokuwa na tija.

"Waliochaguliwa wafanye kazi kama ambavyo kaulimbiu ya Mufti imekuwa ikisema kuwa 'badilika acha mazoea' ili kwenda na kasi ya viongozi wetu wa serikali na kiimani"alisema Omary.

Hata hivyo, aliwataka waliokosa nafasi za uteuzi huo kutoa ushirikano kwa waliopata ili kusaidia kusukuma gurudumu la maendeleo na BAKWATA na taifa kwa ujumla.



Mchuuzi wa matunda aina ya topetope, Robent Magawa, akimuuzia mteja wake, Godfrey Swai katika Mtaa Sango, jijini Dodoma jana. Matunda matatu yaliuzwa kwa Sh.1000. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Waziri awapa tahadhari walimu utitili wa mikopo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, (TAMISEMI), David Silinde, amewataka walimu kujiepusha na utitili wa mikopo isiyokuwa na tija kwao hali inayosababisha wengi wao kukosa ufanisi katika utendaji kazi.

Aliyaseama hayo juzi jijini Dodoma, wakati akifungua kikao cha umoja wa Maofisa Elimu Kata Tanzania, kinachofanyika kwa siku mbili.

Alisema kuwa, Ofisi yake imebaini kuwa walimu wengi wana mikopo mingi isiyokuwa na tija na kuwasababishia kukosa utulivu wakati wa utekeleza majukumu yao ya kufundisha.

Pia, alisema kuwa walimu wengi kutokana na kuwa na mikopo mingi isiyokuwa na tija imewasababishia kuwa na madeni makubwa yanayowalazimu mishahara yao kutumika kulipa na wao kubaki mikono mitupu.

Kutokana na hali hiyo Silinde, aliwaagiza maofisa Elimu Kata nchini kuhakikisha wanatoa elimu kwa walimu namna ya kuepuka kuingia katika mtego huo wa utitili wa mikopo ambayo haina tija.

"Ofisi yangu imebaini kuwa walimu wanamikopo mingi sana na kutokana na hali hiyo wanashindwa kufanya kazi kwa utulivu kwani wanakuwa wakiwaza madeni ambayo hawana faida nayo.

"Sisi kama serikali hatutaacha kukupa pesa zako za mshahara lakini taasisi za kifedha ndizo zitakazokuwa zinafaidi na sisi hatutakubali kuona kazi inaharibika,"alisema Silinde.

Alisema mwalimu anaweza kuona kukopa milioni 10 ni nyingi lakini baada ya miezi miwili ndipo atakapoona kuwa amejiweka katika mazingira magumu.

Kadhalika, Silinde aliwaagiza maofisa elimu hao wa kata kwenda kusimamia ufundishaji na ujifunzaji hasa kuondoa tatizo la kusoma, kuhesabu na kuandika (KKK).

Kwa upande wake Naibu Katibu Mkuu TAMISEMI, Gelard Mweri, aliwataka maofisa elimu mikoa na wilaya kuhakikisha kuwa wanatoa ushirikiano kwa maofisa elimu kata sambamba na kuwapatia taarifa sahihi ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufasaha.

Vile vile, aliwataka maofisa elimu kata kuhakikisha wanasimamia elimu kuanzia ngazi ya shule za msingi, sekondari pamoja na taasisi za elimu ya watu wazima.

# Umoja Wazalisha Almasi Afrika kuzungumza Kiswahili

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Madini, Dotto Biteko, amesema nchi 19 za Umoja wa Uzalishaji wa Almasi Barani Afrika (ADPA) zimekubaliana kuongeza lugha ya Kiswahili kuwa miongoni mwa lugha za mawasiliano katika jumuiya hiyo.

Aliyasema hayo jana jijini hapa wakati wa Mkutano wa saba wa Mawaziri wa nchi za Afrika zinazozalisha madini hayo ulioganyika kwa njia ya mtandao.

Alisema awali lugha zilizokuwa zikitumika ni Kifaransa, Kiingereza na Kireno.

Aidha, alisema katika mkutano huo wamekubaliana ndani ya miezi sita Kamati Tendaji ya ADPA itafanya marekebisho na maboresho katika mfumo wa menejimenti ya utendaji ya umoja huo.

Biteko alisema pia Tanzania imezialika nchi wanachama na kufanya ukaribisho wa kutumia soko la madini hayo nchini kuuza madini yao.

"Tumeoa ukaribisho wa kutumia soko la almasi, tutaendelea kulisukuma mbele kwa sababu tutakuwa wenyeviti wa ADPA," alisema Biteko.

Biteko alisema wakati Tanzania itakuwa mwenyekiti wa jumuiya hiyo, Makamu Mwenyekiti wa ADPA atakuwa nchi ya Zimbabwe ambaye atashika madaraka ya uenyekiti baada ya Tanzania kumaliza muda wake.

"Zimbabwe itapokea kijiti cha kuongoza jumuiya hiyo baada ya Tanzania ili kusukuma mbele maendeleo ya jumuiya hiyo,"alisema Biteko.

Naye, Waziri wa Madini na Nishati wa Jamhuri ya Namibia, Tom Alweendo wa nchi ambayo imemaliza uenyekiti wake, aliitaka Jumuiya hiyo kupata viongozi shupavu wa Kamati Tendaji watakaosaidia kuweka msukumo katika utekelezaji wa malengo ya jumuiya hiyo.

Aliongeza kuwa, kama wanachama ni lazima wachochee na kuweka mikakati ya kupigania maslahi ya Afrika kwa madini ya Almasi ikiwamo kuzitaka nchi hizo kuhakikisha zinalipa michango yao kwa mujibu wa sheria.





# Bei za mafuta Z'bar zapanda

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) imefanya mabadiliko ya bei za mafuta zilizoanza kutumika rasmi kuanzia jana.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, kwenye ukumbi wa ZURA ulioko Maisara wakati alipokuwa akitoa taarifa kwa umma juu ya mabadiliko ya bei za mafuta, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano ZURA, Mbaraka Hassan Haji, alisema mabadiliko hayo yanatokana na vigezo mbalimbali.

Mbaraka alisema ZURA imepanga bei ikiwamo kuzingatia wastani wa mwenendo wa mabadiliko ya bei za mafuta duniani katika mwezi uliopita kwa lengo la kupata kianzio cha kufanyia mabadiliko ya bei za mafuta kwa mwezi huu.

Pia alisema mamlaka inazingatia gharama za uingizaji mafuta katika Bandari ya Dar es Salaam, thamani ya Sh. ya Tanzania kwa Dola za Kimarekani, gharama za usafiri, bima na 'Premium 'hadi Zanzibar, kodi za serikali na kiwango cha faida kwa wauzaji wa rejareja.

Alisema bei mpya ya petroli ni Sh. 2,165 kwa lita ambayo ni ongezeko la Sh. 139 ya Sh. 2,026 sawa na asilimia 8.86.

Kuhusu dizeli, alisema imeongezeka kwa Sh. 83 kwa lita na itauzwa kwa Sh. 2,124 tofauti na Sh. 2,041 kwa lita kama ilivyokuwa mwezi uliopita. Ongezeko hilo ni asilimia 4.07.

Kwa upande wa mafuta ya taa, bei haijabadilika kutoka ile ya Machi ambayo ni Sh. 1,471 kwa lita. Katika hatua nyingine, Mbaraka alisema ZURA inawasisitiza wananchi wanapokwenda kununua bidhaa hizo, wadai risiti na wanapokutwa na changamoto ikiwamo huduma za mafuta, maji na gesi wawasiliane na mamlaka ili kupata ufumbuzi.



Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi wa Viwango Zanzibar (ZBS), Rahima Ali Bakari, akifafanua jambo kwa waandishi wa habari, mjini Zanzibar jana, kuhusu masuala mbalimbali ya uthibitishaji viwango. **PICHA: HAWA ABDALLAH**

# SMZ yajizatiti kushirikiana na JMT mambo ya maendeleo

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imejizatiti kutoa ushirikiano kwa taasisi za serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuhakikisha wanakaa pamoja ili kujadili mustakbali wa maendeleo kwa pande zote mbili.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, aliyasema hayo juzi alipokutana na viongozi wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, walipofika ofisini kwake, Vuga, kujitambulisha.

Alisema SMZ iko wazi kutekeleza maelekezo ya Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, juu ya kuzidisha ushirikiano kupitia vikao vya pamoja katika kujadilii masuala mbalimbali.

Hemed aliongeza kuwa serikali iko tayari kusaidia watendaji wa tume hiyo pale watapohitaji msaada ili kuwawezesha Watanzania kupata haki zao stahiki katika tume hiyo.

Akizungumza kuhusiana na suala la ajira Hemed alisema serikali itazingatia kufuatwa kwa taratibu ili kutoa ajira pande zote mbili za Muungano.

Aliushukuru uongozi wa tume hiyo kwa utekelezaji wa majukumu yake na kusema kuwa serikali ya awamu ya nane Zanzibar inayoongozwa na Rais Dk. Hussein Mwinyi, imejipanga kuhakikisha wananchi wanafaidika na matunda ya serikali yao. Mapema, Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Jaji Mstaafu Mathew Mwaimu, alisema ujio wao umelenga kuongeza ushirikiano wa karibu kwa vile Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar na ile ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndizo zinazoratibu masuala ya Muungano.

Aliongeza kuwa Tume ya Haki za Binadamu Tanzania ina wajibu wa kusimamia haki za kijamii nchini ili kuongeza kasi ya maendeleo.

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora yenye makao makuu jijini Dodoma, ikiwa pia na ofisi yake Zanzibar, ina matawi mengine katika maeneo mbalimbali ikiwamo Pemba, Lindi, Mwanza na Dar es Salaam.

# Taasisi yakiri gharama kubwa vipimo

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TAASISI ya Viwango Zanzibar (ZBS) imekiri kuwapo kwa gharama kubwa za upimaji wa bidhaa hali inayosababisha wajasiriamali wengi kushindwa kumudu gharama hizo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkurugenzi Mkuu wa taasisi hiyo, Rahma Ali Bakari, alisema licha ya kuondolewa kwa gharama za ukaguzi, changamoto iliyopo ni gharama za upimaji wa viwango vya bidhaa za vyakula .

Alisema ukubwa wa gharama hizo unatokana na taasisi hiyo kutokamilika kwa maabara inayohusiana na upimaji wa bidhaa ya vyakula na kusababisha sampuli hizo za vyakula kupelekwa katika mabaara zingine nje ya taasisi hiyo.

"Kutokana na gharama hizo kuwa kubwa ZBS inashindwa kumudu kuwasaidia wajasiliamali wote na wao wenyewe kushindwa kubeba gharama hizo badala yake kuwaondolea gharama zingine kwa wajasiriamali ambao wamekidhi vigezo," alisema.

Alisema gharama za upimaji kwa upande wa bidhaa za vyakula kimelea kimoja zinafikia Dola 50 za Marekani na katika bidhaa ya chakula inahitajika kupimwa vimelea zaidi ya vitatu.

"Kweli gharama kubwa na wajasiriamali hawaziwezi. Licha ya ZBS kuchukua hatua mbalimbali ili kuwapunguzia mzigo, katika suala la upimaji hili tumeshindwa na hii inatokana na vipimo vingine kupatikana nje ya maabara ya ZBS," alisema.

Pia alisema taasisi hiyo katika mwaka ujao wa fedha, imeandaa mkakati maalum wa kuwasaidia wajasiriamali kwa kuwagawa katika makundi hususan kwa wale ambao wamekidhi vigezo.

Alisema changamoto kubwa iliyopo kwa wajasiriamali ni kutokuwa na maeneo maalum ya kufanyia biashara zao hali inayosababisha hata ZBS kupata wakati mgumu katika kufanya ukaguzi bidhaa zao.

Hata hivyo, alizishauri mamlaka zingine nchini kuwasaidia wajasiriamali kufikia viwango vya ubora wa bidhaa zao wanazotengeneza ili wazalishe bidhaa zenye ubora na kuepusha gharama za upimaji wa mara kwa mara pale inapogundulika kuwa hazina ubora.



**KHLOE ETI RAHA JIPE MWENYEWE** Ukurasa.14





## UTATA WATANDA

# Ben Pol kuomba talaka kortini

MASHABIKI wa muziki na wafuasi wa msanii wa Bongofleva, Ben Pol, wamejikuta wakihoji sababu ambazo zimemfanya kuomba talaka kwa mke wake Arnelisa.

Wiki hii kumeripotiwa habari kuwa mwimbaji huyo wa muziki wa kimahaba amewasilisha mahakamani maombi ya kuvunja ndoa yake.

Kinachoshangaza wengi mpaka sasa ni kwa nini anachukua uamuzi mgumu katika muda mfupi, tangu aamue kubadili dini na kuwa Muislam.

Katika taarifa zilizosambaa mitandaoni zinadai, Ben Pol amefungua shauri la kuomba talaka katika mahakama moja ya mwanzo jijini Dar es Salaam, akitaka kumtaliki Mke wake Anerlisa ambaye ni raia wa Kenya.

Hata hivyo, sababu za kuchukua uamuzi huo umebaki kuwa siri.

Ben Pol na Anerlisa walifunga ndoa mwishoni mwa mwezi Mei, mwaka 2020 katika Kanisa Katoliki la St. Gaspar Mbezi Beach.

“Ukiona mwanamume anafungua keshi ya kuomba talaka kwa mke wake, basi tambua kuna mambo yamemfika kooni. Inawezekana Ben Pol kuna mengi aliyavumilia katika ndoa yao na sasa yamemshinda,” amesema Amina Ngulangwa mkazi wa Gongolamboto.

Aidha mwingine amehoji “Ni nini kimemkumba mwamba , au alitaka mabilioni ya Anerlisa akatolewa nje? Ikumbukwe penzi hili ni kama lilimtoa katika ramani ya mziki,”

Aidha, idadi kubwa ya mashabiki wake wanataka mwanamuziki huyo kujitokeza kuweka wazi ili sitofahamu hiyo imalizike na sio kufanya kuwa siri.

BASI SAWA

## Unene wa Msechu si kitu

MSANII wa muziki, Peter Msechu ambaye anaandamwa kutokana na kuongezeka uzito kupita kiasi, ameibuka na kusema umbo lake ndio 'Brandi' yake na hawezi kubadilika.

Akizungumza na EATV, Msechu amesema maneno hayo hayatamwathiri chochote, huku maisha yake yataendelea kuwa mazuri kila kukicha.

"Hakuna kitu kinachoniathiri nitabakia kuwa Msechu na brand yangu itabaki hivi hivi na nitaendelea kuishi maisha yangu na kuzingatia kula vizuri, kuishi vizuri, kufanya mazoezi na sina magonjwa nyemelezi" amesema.



## Eti Anjella bado kinda?

MWANAMUZIKI wa kike kutoka lebo ya Konde Gang, Anjella, amesema watu wasianze kumsumbua kwani bado ana umri wa miaka 19, umri ambao sawa na mtoto.

Anjella amesema kwa sasa hayupo kwenye uhusiano wa kimapenzi kwa sababu wanaume wanahitaji uvumilivu pia yeye ni mtu wa dini hivyo anazingatia maadili.

"Ni kweli sina mpenzi na sipo kwenye uhusiano, kwanza mimi ni binti mdogo nina miaka 19 sitakiwi kujihusisha na hayo mambo siwezi ku-control mapenzi na kazi kwa wakati mmoja kwa hiyo itabidi nipige kazi na nilishaapa sitaki kuja kufa masikini hivyo lazima nipambane" amesema.





## Gigy Money atibua mambo

MSANII wa muziki na filamu nchini, Gigy Money, ametibua hali ya hewa baada kuomba hata yeye afunguliwe kifungo chake ili aanze kufuata sheria.

Gigy Money, alifungiwa miezi sita kushiriki kazi yoyote na Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA) baada ya kukiuka maadili wakati wa shoo yake moja.

Kufuatia hutuba ya Rais Samia Suluhu Hassan akitaka vyombo vya habari vilivyofungiwa vifunguliwe, msanii huyo aliandika katika mtandao wa Instagram kuwa hata yeye pia afunguliwe.

"Na mimi nifunguliwe jamani, kazi inaendelea mama". ameandika msanii huyo.



## Lulu Diva anashangaa, wote wanamshangaa

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Lulu Diva, amemshangaa msanii mwenzake Ben Pol kuomba talaka kwa mkewe Anerlisa Muigai, akisema yeye analilia kuingia katika ndoa hata kesho.

Lulu Diva ameandika kupitia akaunti yake ya Instagram baada ya kutoka taarifa ya msanii Ben Pol kufungua shauri Mahakamani kudai talaka kwa mkewe huyo ambaye raia wa Kenya.

"Ila haya mapenzi hayana adabu mimi nipo single ndio nataka kuingia mara nasikia ndugu yangu Ben Pol anadai talaka anataka kutoka, sasa niache au niendelee kutafuta mpenzi" ameandika msanii Lulu Diva

## 5 alizokamua King Geovani




**Na Adam Fungamwango**

ILIKUWA ni wiki nyingine ngumu kwa mashabiki wa muziki wa dansi nchini Tanzania, baada ya kutangazwa habari za kifo cha mwanamuziki mahiri wa Chuchu Sound, King Geovani.

Mwanamuziki huyo ambaye ni mpiga solo, alifariki ghafla mwanzoni mwa wiki hii baada ya kupatwa na shinikizo la damu kwa mujibu wa mwanamuziki mwenzake, King Dodoo.

King Geovani amefariki wakati akiwa mmoja wa wanamuziki wenye asili ya Congo walioshiriki kutunga nyimbo za kumuenzi aliyekuwa Rais wa Tanzania, Dk John Magufuli, aliyefariki dunia Machi 17, mwaka huu.

King Geovani, mwenye asili ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo alianza kupata umaarufu mwanzoni mwa miaka ya 2000 alipojiunga na Chuchu Sound, bendi ndogo ambayo ilitikisa nchi kwa nyimbo zake kali, zikiwamo zile za mduara, huku nyingi yeye alipiga gitaa ongozi la solo.

Akiwa na mmiliki na kiongozi wa bendi hiyo,Yusuph Chuchu, Mao Santiago, Gabby Katanga ambao wote ni marehemu, kukiwa pia na Jenico Flower pamoja na Omari Mkali, walitengeneza bendi iliyozikisa vigogo.

Hizi ni baadhi ya nyimbo zilizotamba, ambazo hayati King Geovani alipiga solo.

**Sitishiki**

"Sitishiki mimi sibabaiki, niko freshi na niko fiti...Si kwa mzizi si hirizi jambo lilo huwezi...si rahisi kuchota maji kwa pakacha kuliko yeye kuniacha..." Hayo ni baadhi ya maneno kwenye wimbo huo.

Hizi ni baadhi ya nyimbo za mwanzo kabisa zilizoanza kuipa umaarufu bendi hiyo. Upo kwenye mtindo wa mduara. Utamu wa nyimbo hizi huchagizwa na sauti ya Omari Mkali kwenye vibwagizo, lakini pia linapoachia solo la marehemu, Mkali hupagawa na kuita kwa sauti "King Geovaniii."

**Marafiki**

Huu ni moja ya nyimbo chache za Chuchu ambazo hazipo kwenye mtindo mduara lakini zikapata umaarufu mkubwa.

Chuchu walikuwa wakichanganya nyimbo za mitindo mbalimbali, lakini zile za mduara kwa kiasi kikubwa ndizo zilizofanya vizuri. 'Marafiki' ni wimbo ambao haukuwa na mduara, lakini solo la King Geovani na sauti tamu ya Jenico Flower ulifanya wimbo huo kupendwa sana.

**Hodi hodi**

"Hodi hodi, wana Chuchu ooo, twaingia tena 2001." Ilikuwa ni albamu nyingine ya pili waliyoingia nayo ambayo walitaka kuthibitisha kuwa ile ya kwanza hawakubahatisha. Na kweli, ikashika vilivyo. Baada ya hapo Chuchu Sound ikawa ni bendi tishio na yenye mashabiki wengi kila kona ya nchi. Geovani naye alionekana pia ni hatari kwa wapiga solo wengine.

**Usione Vyaelea**

Wimbo huu ni mfululizo wa nyimbo za mduara ambazo walikuwa wakizitoa Chuchu Sound na kufanya vema mno. Hakuna tena mashabiki aliokuwa na wasiwasi nao. King Geovani naye alizidi kuonyesha ufundi wake kiasi cha bendi nyingi kumtamani.

**Shanuo**

Ni wimbo mkali wa mduara ambao nao ulitikisa hasa. Kwa bahati mbaya sana wimbo huu ni moja kati ya zile za mwisho wa uhai wa bendi hii, kwani pamoja na yote ulirekodiwa wakati baadhi ya wanamuziki wake wakiwa wameshaanza kusambaratika kwa kuchukuliwa na bendi zingine. King Geovani yeye alikuwapo na kupiga solo kama kawaida.

"Salama ni salam wala sina gharama, kutenda mtende nyie, tukitenda siye lawama." Ni baadhi ya maneno yaliyomo kwenye wimbo huo.

## Matatizo ya Mapacha; Mlamba asali, huchonga mzinga

**Na Adam Fungamwango**

'MATATIZO ya Pacha' ni filamu ambayo pamoja na kwamba ina ucheshi ndani yake kwa kuigizwa na baadhi ya wasanii kama mzee Majuto, lakini ina mafundisho makubwa ndani yake.

Unaweza ukadhani ni ngumu kutokea, lakini kwenye jamii zetu za Kiafrika, kuna mambo hujitokeza mpaka unaweza kushangaa kama ni kweli au hadithi tu za kusadikika.

Filamu hii ina imechezwa na mzee Majuto, mzee Korongo, mzee Muhogo Mchungu na wengine wengi.

Inaanza kwa mtoto wa mzee Muhogo Mchungu anataka kuoa. Anakwenda kwa mzee Korongo. Mzee Korongo ana wapwa zake mapacha ambao wanaishi mbali na mji huo.

Kulwa anakwenda kumtembelea mjomba wake mzee Korongo ambako huko anaonekana na kijana wa mzee Muhogo Mchungu anampenda.

Anakwenda kupeleka barua kwa mzee Majuto ambaye anakuwa mshenga. Kulwa anakubali kuolewa na kijana wa mzee Muhogo Mchungu. Siku chache kabla ya harusi, Kulwa anaugua na kusababisha ndoa kuwa mashakani kufungwa au kuahirishwa kwa muda.

Hilo linawatisha mzee Majuto na mzee Korongo. Kwa sababu anajua kuwa binti yule ana ndugu yake pacha ambaye ni doto, wanapanga mpango wa kwenda kumchukua Doto nyumbani kwao na kuja kumuozesha ili wasikose mahari yao. Hilo linafanyika. Hata hivyo Doto anaambiwa kuwa wanafanya hivyo kwa sababu dada yake ni mgonjwa, lakini akipona yeye anaondoka hapo kurudi kwao, na Kulwa anakuja kuchukua nafasi yake bila mtu yoyote kujua. Kulwa anarudishwa kwao na doto analetwa, ndoa inafungwa.

Baada ya mwezi mmoja, Kulwa anapona na akili inamrudia. Anaanza kukumbuka kuwa ana mchumba na siku chache kabla ndoa akaanza kuumwa. Alipouliza na kufuatilia akaambiwa kila kitu kilichotokea. Doto naye anakwenda kuambiwa kuwa dada yake amepona, hivyo wafanye kama walivyoahidiana, aondoke hapo na kurudi kwao, Kulwa achukua nafasi yake. Doto amenogewa, hataki kuondoka.

Unatokea mzozo mkubwa mpaka siri inafichukua kuwa kuna mpango kabambe ulichezwa. Hapo ndipo kijiji kizima kikajua kuwa kumbe mchumba na alioolewa walikuwa ni watu wawili tofauti ambao ni mapacha.





# Davido, Burna Boy waongoza Afrika

WANAMUZIKI wa Nigeria, Davido, Burna Boy, Wizkid na Mr Eazi wamekuwa kama alama ya bara la Afrika mwaka 2021.

Kulingana na jarida la Forbes, wasanii hao nyota wanaongoza katika orodha ya wasanii wa muziki katika bara hilo.

Jarida hilo limewataja wasanii hao kuwa wana uwezo mkubwa wa kuwa matajiri wa baadae endapo wataongeza juhudi zao za kufanya kazi pamoja na kubuni vyanzo vingine vya mapato.



## Awilo Longomba kushiriki filamu Tanzania

MWANAMUZIKI mkongwe wa muziki wa dansi kutoka DRC, Awilo Longomba, ametua nchini Tanzania kwa ajili ya kushiriki filamu ya A Life To Regrt.

Filamu hiyo ambayo inatengenezwa na kampuni ya Bjb films itagusa matukio mbalimbali ndani ya jamii za Kiafrika.

Akizungumza baada ya kuwasili uwanja wa ndege, Awilo amesema Watanzania ni watu wema na ndio maana anapofanya ziara yake huwa na furaha.

## Master P amwombea DMX

MWANAMUZIKI mkongwe wa marekani, Master P, amejikita kumwombea msanii mwenzake DMX, huku akiwataka rapa wengine kujifunza kwa kufanya kazi zenye mtazamo mzuri katika jamii.

DMX anapigania maisha yake akiwa hospitali moja mjini New York, kwa kile kinachodaiwa matumizi makubwa ya dawa za kulevya.

Master P amesema anachukia jinsi wanamuziki wa hip-hop wanasubiri hadi kitu kibaya kimtokee mmoja wao, ndipo wanajitokeza kutoa msaada, hivyo amefikiria kunahitajika kuunda umoja wa kusaidia wasanii kupitia nyakati ngumu, hasa kuelimisha matumizi ya dawa za kulevya.






## Khloe eti raha jipe mwenyewe

KHLOE Kardashian ameamua kujitokeza kuzungumzia kuvuja kwa picha yake katika mitandao ya kijamii na kuibua gumzo na mijadala mikali.

Mrembo huyo na mwanamitindo, picha yake ambayo alionekana yupo bafuni akioga, ilichapishwa kimakosa mtandaoni na kusababisha mashabiki wake kumlalamikia kutokana na kitendo hicho kisicho na maadili.

Khloe amesema kama kuna mtu amechukua picha yake kwa nia mbaya hana sababu ya kuongea, lakini yeye binafsi ana haki ya kufanya jambo lolote bila kujadiliwa, na kila mtu anaweza kumuuliza suala hilo," amesema Khloe.

## Chris Brown afanya 'sapraizi' Bongo

MWANAMUZIKI wa Marekani, Chris Brown, amemtuliza shabiki wake wa Tanzania, baada ya kuposti daladala aina ya kipanya ikipita katika maeneo ya mkoa wa Mwanza.

Video fupi ambayo inaonyesha daladala hiyo ambayo mbele imeandikwa Kisesa kwenda Nyashishi, ikitembea kwa kasi huku sauti ya mtu ikisikika akisema anamtumia Chris Brown ili aiweke katika mtandao wake wa kijamii.

Inawezekana Brown aliamua kuiposti kutokana na gari hilo kupambwa na picha zake katika kioo cha nyuma, hivyo kuonekana imemvutia.



MAKALA

# Wajua mfadhaiko baada kujifungua unamtuma mama kumdhuru mtoto?



Christina Mwakangale

KUJIFUNGUA salama na mama kukutana na mtoto wake aliyembeba kwa miezi tisa ni jambo linalomfurahisha kila mmoja si mama mzazi pekee bali pia familia, wahudumu wa afya na jamii inayomzunguka ikimtakia heri.

Lakini, misukosuko inayoambatana na uzazi inaweza kumletea mama kuchanyanyikiwa au mfadhaiko unaokuja baada ya kujifungua unaojulikana kitaalamu kama 'postnatal depression', hali hii humkumba mwanawake yeyote muda mfupi baada ya kujifungua na kwamba ni kati ya aina za msongo wa mawazo, ambayo huweza kumpata mama mzazi baada ya kupata mtoto.

Wataalamu wanasema ni tatizo sugu na huathiri mwanamke moja kati ya 10, kwa mwaka baada ya kujifungua, pia ni hali ambayo huwapata kinababa pia.

Hali hiyo humfanya mama kupatwa na huzuni, wasiwasi, hasira, woga, furaha kuzidi na hofu kutokana na hisia zitokanazo na vichocheo vinavyozalishwa mwilini kuwa katika kiwango kikubwa na kuleta athari.

Inatarajiwa mwanamke aliyebeba ujauzito kwa miezi tisa na kupitia hali tofauti za machungu, hadi kujifungua, ndivyo ambavyo anajenga kiwango kikubwa cha mapenzi kwa mwanae na kumlinda.

Kwa wanyama wote jamii ya mamalia wanaozaa na kunyonyesha, akiwamo binadamu, huwa ni wakali na hata kumdhuru yeyote ambaye atajaribu kuhatarisha usalama wa maisha ya mwanae.

Hii pia inashuhudiwa hata kwa wanyama wafugwao au wale wa porini, mfano paka na simba, iwapo yeyote akijaribu kumshika au kumuiba mwanae, huweza kumjeruhi, lakini hali ya upendo, mapenzi ya mama kumlinda mwanae, huweza kuwa kinyume baada ya kupata mfadhaiko mara baada ya kujifungua na kumuona mwanae adui.

Hiyo husababisha hata kumdhuru, kisha jamii inayomzunguka kubaki ni mshangao na kwamba matukio kadhaa yanayoshuhudiwa kwenye jamii, ikiwamo la mama aliyejaribu kumdhuru mwanae, mwaka jana, mkoani Kagera, ilishuhudiwa mama akimtupa mwanae wa umri wa miezi sita, kwenye shimo la choo.

Mtoto huyo alinusurika baada ya kuokolewa na askari wa Jeshi la Zimamoto, ambaye baadae alipewa tuzo na kupandishwa cheo.

**MFADHAIKO NI NINI?**

Mfadhaiko huo unaokuja baada ya kujifungua ni nini? Kwa mujibu wa Dk. Isaac Maro anayetoa ufafanuzi kuhusu tatizo hilo katika moja ya vipindi vya redio, anasema waliotoka kujifungua hupata tatizo hilo na lisipodhibitiwa linaweza kuleta madhara.

Anasema kwa kawaida inatarajiwa mama amlinde mwanae baada kupitia hali tofauti za machungu wakati wa ujauzito hadi kujifungua na kunamfanya kufungamana na mwanae zaidi, kuliko mtu mwingine.

"Hali alizopitia mama kipindi cha ujauzito, uchungu na kujifungua ndizo ambazo zinamfanya mama kumpenda na kufungamana na mtoto wake kuliko mtu mwingine, lakini anaweza kupata msongo wa mawazo, sonona na hisia ambazo zinamsababishia kumzira mtoto na kujiona mkosaji." Anasema Dk. Maro.

Anabainisha kuwa mama ambaye hapati ukaribu wa baba, jamii, pamoja na familia yake baada ya kujifungua, hupata tatizo hilo na kuleta madhara kwa wanaomzunguka au kumdhuru mtoto na kushauri kuwa mwanamke aliyetoka kujifungua akionyesha dalili za ugonjwa wa tatizo hili anapaswa kupata ushauri mapema.

Anasema huenda wanawake wote waliotoka kujifungua wanapitia hali hiyo inayoitwa 'baby blues' ambayo hutokea kwa siku mbili hadi tatu.

Dk. Maro akifafanua zaidi anasema vichocheo (hormones) vinapozidi husababisha mjamzito aonekane wa aina fulani, akipata woga uliopitiliza au wasiwasi na kwamba ukubwa wa tatizo husababisha mama kutokuwa na raha, kushindwa kukaa na mtoto hata kumtupa.

"Utasikia matukio kadhaa mtoto ametupwa au ameokotwa mahali lazima atakuwa kati ya hali hii. Ukiuliza watasema alikuwa na sonona kwa kawaida mama anavyopitia machungu ndivyo atavyotakiwa amlinde mtoto wake, ikiwa kinyume hii ni sonona.

"Hasira anakuwa nazo anajiona yeye si mama mzuri, hana thamani anashindwa kupumzika, na kuhisi kama kuna kitu kibaya kinatokea ana paniki au kuhamaki au anataka kujiumiza mwenyewe au mtoto, pengine kujiua au kuua," anasema Dk. Maro na kuongeza: "Ushauri na nasaha ndiyo utasaidia. Hali hii ikidumu muda mrefu husababisha afanye matendo ya kushangaza jamii."

Mtaalamu bingwa wa afya ya akili na magonjwa ya akili kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili, Dk. Saidi Kuganda, anasema sonona ni maradhi ya akili ambayo mama anayejifungua anaweza kupata matatizo hayo.

Anaeleza kuwa makundi hayo yapo kwenye makundi mawili na kwamba kuna madogo yasiyohusisha kuchanganyikiwa akili na kundi jingine ni maradhi makubwa yanayohusisha kuchanganyikiwa.

Anasema kati ya dalili ambazo zinatajwa kuwa mama aliyetoka kujifungua ana mfadhaiko ni pamoja na kukosa usingizi, kujiona dhaifu, kukosa furaha, wakati fulani kutokwa na machozi wiki ya kwanza baada ya kupata mtoto.

Anaongeza kuwa pia hali hiyo inaweza kujitokeza kipindi chochote ndani ya mwaka mmoja baada ya kujifungua na wengi wao hawajui kuwa wana tatizo hilo.

Akiendeleza kuzungumzia maradhi ya akili Kuganda anasema kuwa kundi la magonjwa madogo ya akili ni pamoja na walio na dalili kama vile hasira, wivu, wasiwasi, woga, sonona, huzuni pamoja na msongo wa mawazo.

Anasema mwenye hofu, wasiwasi na kushindwa kujieleza au kujitokeza mbele ya hadhira, naye pia ana maradhi ya akili na kubainisha kuwa kukosekana utulivu kiuchumi ili kujikwamua humletea mtu msongo wa mawazo.

Bingwa anaeleza kuwa ustawi na mwenendo wa binadamu hasa akishindwa kujikimu na kukabiliana na changamoto, humfanya ashindwe kujiamini, kujieleza mbele za watu kutokana na hisia hasi au hitilafu zilizopo kwenye ufahamu wake.

Anabainisha kwamba maradhi ya akili yasiyohusisha kuchanganyikiwa ni mengi zaidi na binadamu anayapitia kila wakati ikilinganishwa na kundi linguine na kuongeza:"Kutokana na uwezo wa kiakili kuyakabili masuala yanayomkumba ndani ya jamii, wengi wetu hatupotezi uwezo wa ufahamu kiakili."

Anaeleza kuwa mtu anaposhindwa kuyakabili anakasirika, kuwa na hasira kupindukia na kuwa hatari kwenye jamii, anasema Dk. Kuganda.

Anasema binadamu akibadili mwenendo wa namna anavyoishi kama alivyozoeleka kila siku, cha kujiuliza ni akili yake ipo timamu? Anaeleza kuwa jamii inapoona mabadiliko ya mtu katika mwenendo wake kitabia kusikoendana na mazingira, huanza kumpa majina ambayo humtaja kama karukwa na akili, chizi, mwehu, mwendawazimu, kichaa, kachanganyikiwa kabla ya wataalamu kuthibitisha.

Kuhusu hisia hasi, Dk. Kuganda anasema wivu hutokea katika maisha ya binadamu ya kila siku na kwamba kikubwa ni namna ya kukabiliana na hali hiyo, ili isigeuke maradhi ya akili.

# Luxor inaposhangaza dunia

## ■Kuna miji, makaburi ya wafalme wa Misri



Wataalam wa mambo ya kale wakifungua moja ya jeneza lililopatikana kwenye kaburi.

MISRI inatajwa kama taifa la kale duniani ambalo ustaarabu wake umezidi kushangaza kutoka ujenzi wa mapiramidi hadi nyumba zilizojengwa na watu wa enzi hizo.

Hivi karibuni wataalamu wa historia ya nchini humo wamegundua mji wa kushangaza ambao ulikuwapo zaidi ya miaka 3,400 wakati wa muda wa farao.

Nyumba hizo ambazo zilijengwa kwa kutumia mawe mazito zilionekana imara licha ya kuwa na muda mrefu tangu kujengwa kwake.

Mji huo umepatikana katika eneo la Luxor ambalo kumegundulika vitu vingi vya kale ikiwamo makaburi ya mafarao wengi waliotawala Misri ya kale.

Uzinduzi huo umetajwa kuwa muhimu tangu kugunduliwa kwa kaburi la kale la Tutankhamun.

Wana akiolojia hao ambao walikuwa wakitafuta hekalu katika eneo hilo la jangwa, wakati wakiendelea na kazi hiyo ghafla walikutana na kitu ambacho kiliwashangaza wengi, kwani eneo hilo lilionekana kuwa na nyumba nyingi zinazoaminika za watu wa kawaida.

Eneo hilo lilizungukwa na ukuta wa nyumba zilizoonekana kuwa imara zaidi, licha ya baadhi ya kuta zake kuonekana kupotea kutokana na mabadiliko ya kimazingira.

Katika ugunduzi huyo ndani ya vyumba vilivyokuwa na vitu ambavyo Wamisri wa kale walikuwa wakitumia kila siku katika maisha yao.

Baadhi ya vitu vilivyoonekana ni Pete na vyungu vilivyochorwa kwa rangi na kugongewa muhuri wa farao ambaye kipindi hicho alikuwa na nguvu kubwa.

Pia kulikutwa na duka la kuuza mikate katika eneo la jirani ambapo ni ushahidi kuwa chakula hicho kilikuwa kinapendwa watu wengi,

Baadhi ya vyumba vilikutwa na meza za kuandalia vyakula pamoja na sehemu nyingine kulikuwa na ishara ya shughuli za kiwanda.

"Inaonekana kuwa wakazi wa eneo hilo walikuwa wanajishughulisha kutengeneza mapambo ya maeneo ya kuzikia na hekaluni," anasema mtaalamu mmoja.

Uzinduzi huo ulikuwa na taarifa nyingi hata kuhusu majibu ya kwanini eneo hilo lilitelekezwa na watu wake.

Mji huu uliohifadhiwa vizuri umeelezewa kuwa kumbukumbu ya historia ya Misri.

**KITOVU CHA USTAARABU**

Wana akiolojia nchini Misri wametoa ushahidi kwamba Luxor ulikuwa mji wa kistaarabu baada ya kugundulika makaburi mapya ambayo hayakuwa yamekaguliwa awali.

Moja ya kaburi ulimokuwa mwili huo wa binadamu unaaminiwa kuwa ule wa ofisa kutoka ufalme wa Misri wa miaka 3,500 iliyopita.

Makaburi hayo yako eneo la Draa Abul Naga Necropolis, eneo ambalo ni maarufu kwa mahekalu yake na makaburi.

Eneo hilo liko karibu na bonde la wafalme ambapo wengi wa Mafarao wa Misri walizikwa.

Wizara inayohusika mambo ya kale nchini humo inasema kuwa makaburi hayo yalikuwa yamegunduliwa na mwanaakiolojia wa Ujerumani miaka ya tisini iliyopita, lakini ilibaki imefungwa hadi hivi karibuni walipoamua kuyafungua.

Wataalam wa mambo ya kale wamechimbua sehemu ya mabaki ya sanamu linalokadiriwa kuchongwa miaka 3000 ya mfalme wa zamani ambaye inaaminika alikuwa babu wa mfalme maarufu, Tut (Tutankhamun).

Mkuu wa maswala ya kale Misri, Zahi Hawass, anasema sanamu ya Amenhotep III (wa tatu) iligundulika mahali palipokuwa na makazi yake katika mji wa kusini wa Luxor. Hawass aanasema mabaki hayo yanaonyesha Amenhotep akiwa amekaa katika kiti cha ufalme.

Wataalam wanaamini sanamu kamili ilikuwa na ukubwa wa karibu mita tatu.

Farao Amenhotep III alitawala ufalme wa Misri wakati wa kilele cha ustaarabu kutoka miaka ya 1390 hadi 1350 BC. Ufalme huo ulikuwa umeenea kutoka kaskazini ya Sudan ya sasa mpaka Syria.

Mjukuu wake, Mfalme Tut, alivutia macho ya dunia nzima baada ya wataalam kugundua kaburi lake likiwa limejaa vito vya thamani. Mfalme huyo kijana wa chini ya miaka 20 alifariki 1324 BC.



Wataalam wakifanya utafiti kugundua mali kale jangwani.



Mji wa  kale uliogunduliwa eneo la Luxor.

HABARI KIMATAIFA

# Wakuu SADC walaani uasi Msumbiji

**Maputo,** MSUMBIJI

VIONGOZI wa mataifa ya Kusini mwa Afrika, wametoa taarifa ya pamoja wakielezea wasiwasi wao, kuhusu machafuko ya makundi ya itikadi kali yanayoendelea Kaskazini mwa Msumbiji.

Taarifa ya pamoja inayoeleezea hali hiyo na kusababisha vifo vya maelfu ya watu na wengine wengi kuyakimbia makazi yao.

Rais wa Botswana, Malawi, Afrika Kusini na Zimbabwe walikutana na Rais Felipe Nyusi wa Msumbiji, katika mji mkuu wa nchi hiyo, Maputo.

Mkutano huo, uliangazia suluhu ya machafuko yanayofanywa na kundi la wanamgambo lenye mafungamano na kundi linalojiita Dola la Kiislamu (IS) na kuibua kitisho cha kusambaa machafuko kwenye ukanda huo.

Kulingana na taarifa iliyosambazwa kwenye vyombo vya habari, wakuu hao wa nchi walionyesha wasiwasi wao kuhusiana na mashambulizi ya kigaidi yanayofanywa dhidi ya raia wasio na hatia.

Taarifa ilisema, wanawake na watoto wanaathiriwa na machafuko hayo katika jimbo la Cabo Delgado.

Viongozi hao waliokutana ambao ni sehemu ya mataifa 16 ya Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC), walisema wanatarajia kukutana kwenye mkutano mwingine wa kilele utakaojadili mzozo huo Aprili 29, mwaka huu.

Hata hivyo hakukutolewa maelezo zaidi ya hatua za mapambano dhidi ya ugaidi.

Mkutano huo wa kilele unafanyika siku chache tu baada ya waathiriwa 12, ambao huenda ni raia wa kigeni kukatwa vichwa kufuatia shambulizi lililodaiwa kufanywa na kundi la IS, katika mji wa pwani wa Palma uliopo katika jimbo la Cabo Delgado.

Siku moja kabla ya watu hao kukatwa vichwa, Rais Nyusi alitangaza kwamba vikosi vya serikali vimerejesha udhibiti wa mji wa Palma, baada ya makabiliano na waasi waliokuwa wamejihami kwa silaha.

Zaidi ya waasi 100 waliuvamia mji wa Palma, Machi 24 na inakadiriwa takriban watu 50 waliuawa kwenye mapigano hayo ya siku 10

Rais Nyusi alikiri kwamba serikali yake iliomba msaada kutoka mataifa mengine.

Uasi wa kigaidi Msumbiji, ulianza tangu mwaka 2017. Na zaidi ya watu 2,600 huku 670,000 wakiyakimbia makazi yao, kulingana na Umoja wa Mataifa (UN).

**DW**



Kuta za kale ambazo zimegunduliwa na wataalamu nchini Misri ambazo zina zaidi ya miaka 3,400 tangu enzi za farao. **PICHA: BBC**

# Kenya kurejesha chanjo ya Urusi

**Nairobi,** KENYA

KAMPUNI binafsi ya uagizaji chanjo ya Sputnik V, nchini Kenya inafikiria kuzirudisha Urusi, chanjo walizoagiza.

Hatua hiyo inakuja wiki moja baada ya wizara ya afya nchini humo, kupiga marufuku uingizaji, usambazaji na ugawaji wa chanjo dhidi ya corona kutoka vituo binafsi.

Dominic Kariuki, naibu mkurugenzi wa mamlaka ya dawa, alisema kampuni imewaandikia ili kuona uwezekano wa kuzirudisha chanjo hizo.

"Kampuni iko kwenye mchakato rasmi wa kuomba kuzirejesha. Barua tayari imetumwa kwa bodi ya maduka ya dawa na sumu," Kariuki aliliambia Baraza la Seneti.

Katibu Mkuu wa Afya, Rashid Aman alisema amepokea dozi ya kwanza ya chanjo na watapokea dozi ya pili baada ya wiki tatu.

"Hii itawahusu watu 527 pekee, ambao walichanjwa kabla ya marufuku ya chanjo hizo kutangazwa," Aman alisema.

Shirika la Afya Duniani (UN), limependekeza kuwa chanjo zisichanganywe.

**BBC**

## Wanajeshi 11 wa Nigeria wauawa

**Benue,** NIGERIA

JESHI la Nigeria, limesema wanajeshi 11 wameuawa katika shambulio lililofanyika katika jimbo la kati la Benue wakati wa operesheni ya kawaida.

Hayo yanajiri wakati hali ya usalama ikiendelea kuzorota kote Nigeria na vikundi mbalimbali vyenye silaha vikianzisha vurugu.

Jeshi linasema kwamba askari hao, awali walitangazwa kutoweka baada ya kuviziwa na watu wenye silaha.

Timu ya kuwatafuta na uokoaji baadaye iliwakuta wamefariki siku ya Alhamisi katika eneo la Konshisha katika jimbo hilo.

Msemaji wa jeshi la Nigeria, aliiambia Shirika la Habari la Uingereza (BBC), kwamba baadhi ya miili hiyo iliteketezwa.

Alifafanua kuwa shambulio hilo ni uhalifu mbaya na kwamba juhudi zinaendelea kuwasaka wahusika.

Kumekuwa na ripoti kwamba wanajeshi wamewafyatulia risasi kiholela, raia kadhaa kujibu shambulio dhidi ya wanajeshi.

Jeshi limekanusha madai hayo na bado haijafahamika aliyewauwa wanausalama hao.

Jimbo la Benue limekuwa likikabiliwa na ghasia za kikabila, mapigano kati ya wafugaji na wakulima na shughuli za magenge ya wahalifu wenye silaha.

**BBC**

## 'Hewa oksijeni sababu moyo wa Floyd kusimama ghafla'

**Washington,** MAREKANI

UPANDE wa mashtaka katika kesi kuhusu kifo cha Mmarekani mweusi, George Floyd, aliyekufa kwa kugandamiziwa goti shingoni na polisi mzungu, umesema uchunguzi wa kitaalamu umeonyesha kuwa, Floyd alikufa kutokana na kukosa hewa ya oksijeni.

Shahidi wa upande huo, ambaye ni daktari wa mapafu, Martin Tobin, alisema kukosa hewa hiyo ndiko kulikoufanya moyo wa marehemu kusimama na amekosoa madai ya upande wa utetezi wa polisi anayeshutumiwa kumuua Floyd, Derek Chauvin, kwamba, magonjwa aliyokuwa nayo George Floyd yalichangia katika kifo chake.

Mkanda wa video uliosambaa duniani, ulimwonyesha Chauvin akigandamiza goti lake katika shingo ya Floyd kwa muda wa takribani dakika tisa.

**DW**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA INAUZWA

NYUMBA INAUZWA INA VYUMBA VIWILI IPO KIJITONYAMA PLOT NAMBA 712/1 BLOCK 46 DAR ES SALAAM BEI 300M,MAZUNGUMZO YAPO.


Uza,
Chenye Thamani Kubwa
Kwa Kutangaza Nasi
Kwa Bei Poa
Tupigie 0782253676


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**SHAURI LA MADAI NA. 49 MWAKA 2016**
**TRANSPAPER (T) LIMITED...............MDAI**
**DHIDI YA**
**MGT PRINT LIMITED.....................MDAIWA**
**KUITWA SHAURINI**
**Kwa: MGT PRINT LIMITED**

Kwa kuwa mdai aliyetajwa hapo juu, amefungua shauri la madai dhidi yako, shauri ambalo maelezo yake yameelezwa katika nakala za hati za madai zinazopatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Mahakama hii wewe mwenyewe au wakili au mwakilishi wako anayeruhusiwa kisheria, siku ya tarehe 13/4/2021 saa tatu kamili (3:00) asubuhi mbele ya Mheshimiwa Jaji Banzi, kwa ajili ya kujibu madai hayo dhidi yako.

**ANGALIA:** Kama usipohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na Mahakama ikithibitisha kuwa ulipokea taarifa hii ya kuitwa shaurini, basi shauri linaweza kusikilizwa na kuamuliwa bila kuwepo wako. Unaagizwa kuleta vielelezo vyote ambavyo unatarajia kutumia katika utetezi wako siku hiyo.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Chapa ya Mahakama leo tarehe **01 Mwezi APRIL, 2021.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

HAJOKA INTERNATIONAL COMPANY LIMITED ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TATA LPK YENYE NAMBA ZA USAJILI T 917 DMF NA CHASSIS NO. MAT 727006H3R31501 NA ENGINE NO. 6ISBE2303071D64113976. TAARIFA YA POLISI KAH/ TR /RB/ 152/2021.
NA KADI YA GARI AINA YA TATA LPK YENYE NAMBA ZA USAJILI T 921 DMF YENYE CHASSIS NO. MAT 727006H3R31500 NA ENGINE NO. 6ISBE2303071D64113968 KWA YOYOTE ATAKAYEZIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI KAH/TR/RB/152/2021.

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

HAJOKA INTERNATIONAL COMPANY LIMITED ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TATA LPK YENYE NAMBA ZA USAJILI T 913 DMF NA CHASSIS NO. MAT 727028H3A01769 NA ENGINE NO. 6ISBE2303071A64113484 KWA YEYOTE ATAKAYEZIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI KAH/TR/R-B/152/2021

**Magistrates Court( Approved Forms For the Court)**
**GN. NO 943(Contd.)**

**FOMU MIRATHI-2**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya Moshi**
**Kituo cha URU Mkoa Kilimanjaro**
**Usimamizi wa mirathi Na 12/2021**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU VENANCE MALLYA WA URU –NJARI**
**KATIKA SHAURI LA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA ABROGAST MALLYA**

## TANGAZO

(Kanuni ya 52 ya Kanuni za Usimamizi wa Miradhi Mahakama za Mwanzo)
Watu wote wanaoai kuwa na uhusiano wowote /mislay yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 15 mwezi 04 mwaka 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia:
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani Kukaguliwa .
Imepokelewa Leo Tarehe 8 Mwezi 04 Mwaka 2021

..........................................................
**HAKIMU**

## VYETI VIMEPOTEA



**LUCIA JONAS MWALIBE** anatangaza kupotelewa na vyeti vya, **KIDATO CHA NNE** chenye no **S0472/0054.** KIlichotolewa na Baraza la mitihani kupitia **IPINDA SEKONDARI mwaka 2009, ASTASHAHADA** chenye no **IRDP/CRP/10/1027** mwaka **2011** na **STASHAHDA** chenye no. **IRDP/DDP/11/4113** mwaka **2013** vilivyotolewa na CHUO CHA **MIPANGO YA MAENDELEO VIJIJINI.** Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DSM/RGHQ/RB/177785/21.**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)**
**Katika mahakama ya mwanzo MAKOLE**
**Usimamizi wa mirathi 33/2021**

Ombi la **BALVINDER SINGH VIRDI** kuteuliwa kuwa
Msimamizi wa mirathi ya Marehemu **THAKER SINGH**
**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI POPOTE ALIPO.**
Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe **12/4/2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa wasimamizi wa Mirathi hiyo.
Wosia wa Marehemu huyo kama upo Mahakamani waweza kukaguliwa.
Tarehe **8/4/2021**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

THOMAS STEWART MAZOYA anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye jina la DIOCESE OF CENTRAL TANGANYIKA aina ya FEKON namba za usajili MC 615 CJJ . Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: DOD/DOD/RB/38197/2021

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**MIKONGENI**
**Usimamizi wa Mirathi No 6/2021**
**Ombi la EMILIANI APORONAL NOGOLE kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu**
**MKAWA APORONAL MGANDI.**

**KWA HAKIMU MFAWIDHI**
**MAHAKAMA YA MWANZO**
**MIKONGENI S.L.P 2375 MVOMERO**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja
na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe **13/4/2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia ya Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe **09/03/2021**

**IN THE DISTRICT COURT OF MOSHI**
**AT MOSHI**
**CRIMINAL APPEAL NO.30 OF 2020**
**C/F Criminal Case No. 26 of 2020 Originating from Moshi Urban P/Court**
**SOLOMONI SAIDI ALLY..............................APPELLANT**
**VERSUS**
**SHADRACK AMOSI..................RESPONDENT**

**NOTICE OF MENTION/HEARING**
**TO: SHADRACK AMOSI (RESPONDENT)**
Take Notice that the above case has been fixed for mention in the District Court of Moshi on 6th May, 2021.

You are hereby ordered to appear in person or by advocate of agent dully authorized to do so and you are directed to produce on that day any document under which you intend to rely in support of your case.

**TAKE FURTHER NOTICE** that, default of your appearance on that day afore mentioned the court will proceed with the matter in your absence.

Given under my hand and seal of this Court this 1st day of April, 2021
**PRINCIPAL RESIDENT MAGISTRATE**
**MOSHI**


OFISI ZA MATANGAZO Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam. Mob: +255 - 745 700 710. E-mail: advertise@ guardian.co.tz, website: www. ippmedia.com

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MWANZONI ilionekana ni fahari. Wazazi kupata mtoto wa kike. Akaja kuwa msichana mzuri aliyeumbwa akaumbika na kutamaniwa na kila mtu, ni sifa kubwa. Wakati mwingine mzazi hupata hata vizawadi vidogo kutoka kwa watu mbalimbali bila kujua kuwa nia ni kutengeneza mazingira kwa binti yao. Kinyume chake mzee Ngoma na mkewe Fatuma wanapata mtoto wa kike Bishada ambaye anaondokea kuwa tishio kwenye kijiji cha Mtakuja kwa urembo wake.

Badala ya kuwa tija na faraha kwa wazazi wake anageuka kuwa balaa. Wazazi wanakuwa hawana amani kutokana na vitisho mbalimbali ikiwemo kuuawa kutoka kwa watu mbalimbali ndani na nje ya kijiji hicho. Inakuwa tafrani. Kijiji hakikaliki. watu wanatafutana. Moto unawaka. Bishada mwenyewe maisha yake yanakuwa hatarini. Fuatilia kisa hiki ambacho kitakuacha mdomo wazi.

# Aolewe au afe-**1**

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**

"Mwanangu umeshakuwa mkubwa. Siyo mtoto tena. Muda si mrefu na wewe utakuwa kama mimi. Utakuwa na nyumba yako na familia yako, kwa hiyo acha tabia ya kujidekezadekeza hapa."

"Mama una maana gani?"

"Maana yangu ni kwamba jana ulivyokwenda kisimani, huku mzee Fau alikuja hapa kuleta barua ya posa."

"Posa ya nani tena?"

"Kwani humu ndani mtoto wa kike ni nani? Si wewe tu? Au wameniletea mimi mama yako niolewe tena?"

"Mhhh, mama mimi niolewe?"

"Sasa unataka nani aolewe? Niolewe mama yako?" Safari hii mama aliongea kwa ukali kidogo.

Ni sauti iliyofanya binti awe mpole kidogo. Akajifikiria kidogo, lakini akatamka tena.

"Lakini mimi sipo tayari, sitaki kuolewa."

"Kwa hiyo wewe mwanangu, unataka uzeekee hapa? Hebu angalie mwanangu ulivyokuwa mzuri. Wanaume wote kijijini wanakupenda. Wanakusifia. Na wanataka kukuoa. Na kama hivyo barua imekuja jana wewe hutaki. Au una mchumba wako unayemtaka mwenzetu?"

"Sina mama. Sina mchumba yoyote. Siyo kama hawanitaki. Kila siku wananisumbua, lakini mimi mwenyewe bado siko tayari."

"Jiangalie mwanangu. Kuchagua kwingi."

"Siyo hivyo mama."

"Sasa kama hutaki utajua mwenyewe jinsi ya kumwambia baba yako. Leo anataka kwenda kuwaambia wajomba zako ili kesho waifungue."

"Aka mwenzangu, sina mpango huo."

"Haya, hiyari yako, hebu fanya haraka huo mchele kuchagua uwahi kupika, si unaona mawingu hayo, mvua sasa hivi itashuka hapa."

Ulikuwa ni mjadala mfupi kati ya mama na binti yake. Bi. Fatuma alikuwa akimtaarifu binti yake juu ya kuwepo barua ya posa ambayo ililetwa jana yake.

Inaonekana kuwa binti hayupo tayari kuolewa. Pia hana mchumba yoyote yule. Bi. Fatuma anaonekana kutaka binti yake aolewe. Ambacho hataki ni kumlazimisha.

Bi. Fatuma aliolewa na mzee Ngoma na kubahatika kupata watoto watatu. Wawili ambao ni Juma na Rashid ni wa kiume ambao kwa sasa ni wakubwa wa wameanza kujitegemea. Wa mwisho ni Bishada. Walimzaa wakiwa tayari wakiwa watu wazima. Na walishaanza kukata tamaa ya kupata mtoto wa kike.




Kuzaliwa wa Bishada kukaleta furaha kwenye familia. Mama aliona sasa amepata mwenzake. Wa kuongea naye na kubadilshana mawazo kama wanawake. Wa kumsaidia kazi za ndani. Kuchota maji. Kupika na kufua nguo na kufanya kazi zote za kike ambazo alikuwa anazifanya yeye tu.

Bishada alisoma shule ya msingi na sekondari hadi kumaliza kidato cha nne. Hakufanikiwa kuendelea na elimu. Baba yake baada ya hapo hakuwa na uwezo wowote wa kumuendeleza.

Ni msichana aliyejaaliwa uzuri. Hakuwahi kuweka kipodozi chochote kile kwenye mwili wake, wala dawa yoyote kwenye nywele zake. Ndiyo maana ni mzuri na si mrembo.

Aliishi maisha ya kawaida tu ya kijijini kama wasichana wenzake wote. Hata hivuo kulikuwa na utofauti mkubwa kati ya wasichana wa hapo na yeye.

Tangu alipotimiza miaka 10 tu haikuwa siri kuwa yeye hakujijua kuwa ni msichana mzuri. Wakubwa na watoto walianza kumsifia. Hakujua ni kwa nini wanamsifia hivyo. Shuleni ndiyo kabisa. Walimu nao pia walimsifu.

Alipotimiza miaka 18, hakupata sifa tu peke yake. Alitakiwa na yeye mwenyewe. Hakujua chochote kile. Akabaki anashangaa. Wasichana wenzake baadhi hawakutaka kuongozana naye. Walimuonea wivu. Wakipita sehemu yoyote alisifiwa yeye peke yake.

Mama yake Bi. Fatuma alilijua hilo tangu mapema. Akampa elimu ni kwa nini watu wanamsifia na kumtolea macho. Akamwambia ajichunge. Bishada akajichunga. Hii inamuongezea pia thamani. Hakuna kijana au mwanaume yoyote ambaye ameshatembea naye kijijini hapo.

Waharibifu na waroho wakaanza kumchukia. Waoaji, wanaotaka wake kwa ajili ya kujennga familia waliposikia sifa hizo sasa wakaanza kumiminika kuleta barua.

Alikuwa mwembamba, kwenye rangi ya maji ya kunde. Ngozi nyororo mithili ya jongoo. Kichwa chake kilibeba nywele ndefu nyeusi ambazo wakati mwingi aliamua tu kuzikata. Wakati mwingine mama yake anaamua kumsuka mtindo ambayo ilimpendeza.

Pua ndefu ya mchongoko, meno madogo meupe kama theluji na mwanya wa wasatani vilizidi kumthibitisha ubora wa uumbaji kwa msichana huyo. Alikuwa na shepu ya kike hasa, kiasi kwamba kila mwanaume anayekutana naye hata babu kizee, ni lazima amtazame mara mbili mbili na kusifu kazi ya uumbaji uliofanywa kwake.

**Mwanangu Bishada. Kesho jioni tuna kikao. Hicho kikao kinakuhusu wewe. Maongezi yote utayakuta hapo kwa hiyo nakusuhi usiwe mbali. nadhani mama yako amekudokeza kidogo.**

Licha ya sifa zote hizo, hakuwahi kuwa na kiburi au maringo. Aliongea na kucheka na mtu yoyote yule. Wakati mwingine hii iliwafanya baadhi ya wavulana kuona kama vile wako karibuni kukubaliwa.

Akiwa anapika. Bishada bado alikuwa anafikiria jinsi gani atakavyoikataa barua iliyoletwa kwa ajili ya posa.

Hakujua hasa ni nani huyo ambaye alionyesha nia ya kutaka kumuoa. Anachojua wavulana na hata watu wazima tu wengi wameonyesha nia ya kutaka kumuoa. Yeye hakuwa tayari.

Hakuna sababu yoyote ambayo inamfanya afikirie hivyo. Basi tu alidhani muda wake wa kuolewa haujafika.

"Kuolewa ni majaliwa. Kama kuolewa nitaolewa. Lakini siyo sasa hivi. Kwanza jamani ni mpaka mwenyewe umpende mtu mwenyewe anayekuoa?" Alijiuliza mwenyewe, halafu akajijibu. "Yaani uende tu kwa mtu ambaye hata hujampenda, eti kwa sababu tu umeolewa. Mi mbona mpaka sasa sijaona yoyote hapa ambaye nampenda na anaweza kunioa." Alijiambia mwenyewe huku akionja chumvi kwenye wali aliokuwa anapika.

Aliwaza pia jinsi kikao cha kesho kitakachokuwa cha moto. Kitendo cha kukataa aliona kitawakasirisha wazazi wake, pamoja na wajomba zake.

"Hata kama wananipiga basi, lakini nitawapasha." Wakati anaongea hivyo alisikia mlango ukigongwa.

Alikuwa na baba yake mzee Ngoma. "Bishada yupo chumbani kwake, au jikoni." Alisikia sauti ya baba yake ikiuliza.

"Yupo jikoni." Mama yake alijibu.

Wakati akitarajia kuwa ataitwa, alisikia viatu vikijongea jikoni. Mzee Ngoma aliingia jikoni pamoja na moshi mwingi, lakini alijitoma ndani.

"Mwanangu Bishada. Kesho jioni tuna kikao. Hicho kikao kinakuhusu wewe. Maongezi yote utayakuta hapo kwa hiyo nakusuhi usiwe mbali. nadhani mama yako amekudokeza kidogo." Sauti ya mzee Nanga ilikuwa dhahiri masikioni mwa Bishada.

Hakutaka kujibu chochote ambacho kingezua mjadala, au kuweka taswira ya knini kitakwenda kutokea kwenye kikao cha kesho.

"Sawa baba nimekusikia." Alijibu kwa kifupi, lakini akiwa na mawazo mengi kichwani mwake.

**ITANEDELEA JUMAMOSI**

# UNITED YATAJA DAU LA LINGARD




**LONDON,** England

KLABU ya Manchester United wanataka kutumia kikamilifu hamu ya West Ham kumnunua Jesse Lingard msimu huu wa joto na wameweka dau la pauni milioni 30, kwa mujibu wa gazeti la Mirror.

Lingard amekuwa wa kipekee tangu ajiunge na wagonga nyundo hao wa London, Januari, mwaka huu akifunga mabao sita na kutoa pasi za mwisho tatu katika michezo nane tu ya Ligi Kuu England.

United wanataka kutumia nafasi ya ubora wa sasa wa mchezaji huyo kufanya biashara mapema kuelekea katika dirisha kubwa la usajili wa majira ya joto.

West Ham wanavutiwa na huduma ya mchezaji huyo ambaye hana nafasi katika kikosi cha kwanza cha United kwa sasa.

Lakini itakua vigumu kutoa kiasi hicho cha fedha kutokana na kuyumba kwa uchumi kwa klabu nyingi kutokana na mlipuko wa janga la corona.

Lingard ambaye anacheza kwa mkopo hapo West Ham, ameonyesha kiwango cha kuvutia sana, kiasi cha Kocha, David Moyes, kupambana kutaka kumsajili kwa mkataba wa kudumu.

# AC Milan yaikatalia Juventus

**MILAN,** Italia

AC Milan wanaripotiwa kuwa wamekataa kuzingatia uwezekano wa kukamilisha dili la mabadilishano la wachezaji wao na Juventus.

Milan na Juventus walikuwa wanahusishwa na dili la kubadilishana wachezaji, Federico Bernardeschi na Alessio Romagnoli.

Wachezaji hawa wote wamekuwa na wakati mgumu kupokelewa na mashabiki, wakati mikataba yao ikiwa inafikia mwisho Juni 2022.

Kwa mujibu wa Tuttospor, dili hili halitafanyika kwa kuwa wakurugenzi wa Milan hawataki kufanya uhamisho huo kutokana na sababu kadhaa za kiuendeshaji.

Hata hivyo, kwa mujibu wa ripoti, moja ya sababu ni kutofautiana kwa mishahara kati ya wachezaji wanaohusishwa na uhamisho huo wa kubadilishana, kwani Bernardeschi analipwa zaidi ya Romagnoli.

Historia ya shughuli za uhamisho kati ya klabu hizi mbili inatajwa kuwa ni moja ya kigezo, au sababu inayokwamisha suala hili la uhamisho.

Milan pia wanatajwa kuzingatia baadhi ya madili yaliyofanyika huko nyuma ambayo hayakuwa na matokeo mazuri kwa upande wao kwa wachezaji waliotoka Juventus.






# *Hatima ya Neymar, Mbappe haijulikani*

**PARIS,** Ufaransa

MKURUGENZI wa Michezo wa Paris Saint Germain, Leonard, amezungumzia hatima ya wachezaji wao wawili, Neymar na Kylian Mbappe ambao wanahusishwa na kuondoka klabuni hapo.

Wakati Neymar akiwa anahusishwa na kurejea Barcelona, Mpappe amekuwa akihusishwa na klabu ya Real Madrid.

Mikataba ya wachezaji wote wawili inamalizika kipindi cha majira ya joto mwaka 2022 na hivyo kuwafanya PSG kwa sasa kupambana ili kuwashawishi nyota hao kuongeza mikataba.

Leonardo alizungumza hayo baada ya ushindi dhidi ya Bayern Munich, amesema kuwa wana mambo mengi ya kuzungumzia likiwamo suala la mikataba.

"Punde tutazungumzia masuala ya msingi zaidi. Tunafurahi kuzungumzia masuala ya mkataba, lakini kwa sasa tunapaswa kuzingatia mechi dhidi ya Bayern Munich," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

Leonardo pia aliepuka kujibu maswali moja kwa moja kama yalivyoulizwa na Sky Sport Italia, ikiwamo uhalisia wa mchakato wa mkataba mpya wa Neymar kusalia PSG ambao umeonekana kuwa na sintofahamu.

Ripoti za nchini Hispania, zinamtaja Neymar kuwa kwa sasa yupo mbioni kuungana na Lionel Messi pale Barcelona na Mbappe anatarajia kutimiza ndoto yake ya utotoni ya kucheza Real Madrid.

# Aubameyang atemwa kikosi cha kwanza

**LONDON,** England

MIKEL Arteta alisimamia uamuzi wake wa kumtema Pierre-Emerick Aubameyang katika kikosi cha kwanza cha Arsela kwenye wa Ligi ya Europa dhidi ya Slavia Prague na amekisifia kikosi chake kwa kiwango bora, licha ya kupata matokeo ya sare ya 1-1.

Huo ulikuwa ni mchezo wa kwanza wa robo fainali ya michuano hiyo, uliopigwa juzi Alhamisi kwenye dimba la Emirates.

Aubameyang ambaye ni nahodha wa kikosi hicho, aliwekwa benchi Jumamosi wakati Arsenal wakichezea kichapo cha mabao 3-0 kutoka kwa Liverpool na aliingizwa dakika ya 78 kwenye mchezo dhidi ya Slavia.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Gabon alitoa mchango mkubwa wakati Nicolas Pepe akiifungia Arsenal bao dakika nane baadaye na kuhusika kwenye mabao 100 kwenye mashindano yote tangu alipojiunga na Arsenal kutoka Borussia Dortmund Januari, mwaka 2018.

Hata hivyo, Arsenal walishindwa kuondoka na ushindi, baada ya Tomas Holes kusawazisha dakika ya 93 na kuwaaacha washikabunduki hao kuwa na mlima mkubwa wa kupanda kwenye mchezo wao wa marudiano utakaochezwa wiki ijayo.

Licha ya Alexandre Lacazette kukosa nafasi nyingi za wazi na Bukayo Saka kushindwa kufunga wakiwa kwenye nafasi nzuri, Arteta anahisi alichagua kikosi sahihi cha kuanza dhidi ya Slavia.

"Nafikiri wachezaji niliochangua walifanya kila kitu kilichotakiwa," alisema mara baada ya mchezo huo akiwaambia waandishi wa habari.

"Tulicheza kwa kujituma na wachezaji walifanya vizuri. Ingawa tulishindwa kutumia nafasi nyingi za kufunga, lakini tulicheza vizuri."






# RAMOS: MESSI AMEINYIMA MADRID MAKOMBE

**MADRID,** Hispania

SERGIO Ramos amekiri kwamba, Lionel Messi ameifanya Real Madrid wapate tabu sana kwa miaka mingi.

Nahodha huyo wa Real Madrid amebainisha wazi kabisa kuwa Messi amekuwa akiwaweka kwenye wakati mgumu mno wa kushinda mataji kwa kipindi chote alichokuwapo hapo.

Na kwamba, Blancos hao wangeshinda mataji mengi sana kama nahodha huyo wa Barcelona na Argentina asingekuwapo.

Ramos ametoa kauli hiyo wakati leo Jumamosi Madrid itaikaribisha Barcelona kwenye dimba la Alfredo di Stefano katika mchezo wa Clasico wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga.

Katika mchezo wa kwanza, Madrid waliibuka na ushindi wa mabao 3-1, lakini leo Ramos hatakuwapo kwenye mchezo huo kutokana na kuuguza jeraha la kifundo cha mguu.

Ramos ameshinda mataji manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na matano ya LaLiga, lakini Messi ameisadia Barcelona kutwaa mataji 10 na ameleta shida nyingi wakati wa mechi za Classico kwa miaka mingi.

Mchezaji huyo wa Real Madrid aliyecheza mechi nyingi zaidi katika timu hiyo amebainisha hayo kwenye mtirirko wa makala yake ya The Legend of Sergio Ramos.

"Tumepata tabu sana dhidi ya Lionel Messi kwa miaka mingi. "Na labda kama Barcelona isingekuwa na Messi tungeshinda mataji mengi zaidi."

# Benzema: Sasa kila mechi kama fainali

**MADRID,** Hispania

KARIM Benzema anatarajia mbio za kuwania ubingwa wa Hispania kuwa kali, akimaanisha Real Madrid wanatakiwa kucheza kama fainali kwenye kila mchezo uliobaki wa LaLiga, kama wanataka kushinda taji hilo.

Atletico Madrid walionekana msimu huu kuwa na nafasi kubwa ya kushinda taji hilo, lakini kikosi hicho cha Kocha, Diego Simeone kimeshinda mechi nne tu kati ya 10 zilizopita na kuruhusu wapinzani wao kupunguza nafasi.

Barcelona wapo nafasi ya pili kwenye msimamo wakipitwa pointi moja na Atletico wakiwa wamecheza mechi 19 bila kufungwa tangu walipokutana na kichapo cha kushtukiza cha mabao 2-1 ugenini dhidi ya Cadiz, Desemba 5, 2020.

Hata hivyo, Madrid ilishawafunga wapinzani wao hao mara moja kwenye mchezo wa El Clasico msimu huu pale kwenye dimba la Camp Nou, ambao walishinda 3-1.

Benzema anataka matokeo kama hayo wakati watakapokutana tena leo Jumamosi kwenye mchezo wa Clasico.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MBAPPE: FURAHA YANGU NI KUSHINDA

●●● Mshambuliaji huyo aisogeza PSG nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa huku akifurahia pia...

**PARIS,** Ufaransa

KYLIAN Mbappe alikuwa katika hali ya furaha sana baada ya kufunga mabao mawili na kuisadia timu yake Paris Saint-Germain kupata ushindi mzuri wa magoli 3-2 dhidi ya Bayern Munich, kwenye mchezo wa kwanza wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, uliochezwa Jumatano usiku.

Mbappe aliendeleza kasi yake ya kufunga kwenye michuano hiyo mikubwa ya Ulaya na sasa akiwa amefikisha mabao nane katika mechi zake nne zilizopita.

"Juu ya yote hii ni kiwango kizuri cha timu tulichokionyesha," alisema akinukuliwa na RCM Sport.

**"Nilikuwa tayari kunufaika kutoka kwa kazi ya kila mtu, lakini kwangu furaha kubwa ni kuona tuna shinda kila mchezo.**

"Haijalishi ni mabao mangapi yamefungwa, lakini la msingi ni kwamba, tunashinda na kuondoka na ushindi.

"Mchezo wa pili? Kwa kuanza itabidi tucheze vyema dhidi ya Strasbourg wikiendi hii, kisha tutahitaji kushambulia kwa kujiamini, ingawa tunajua kwamba, tunakabiliana na timu kubwa, Bayern Munich.

"Hii ndio Ligi ya Mabingwa Ulaya, kila timu ni kubwa, hivyo unapoingia uwanjani lazima ujipange vizuri."

## ZISIKUPITE

### UNITED YAMTAKA RICE

KLABU ya Manchester United watatathmini uwezekano wa kumsajili kiungo wa kati wa England, Declan Rice, 22, katika mkataba wowote kati yao na West Ham utakaomhusisha Jesse Lingard (28). ***(Athletic - subscription required)***

### LEEDS YAMFUATA AGUERO

LEEDS United imeingia kwenye mbio za kuwania kumsajili mshambuliaji wa Manchester City na Argentina, Sergio Aguero, 32, wakati mkataba wake utakapokamilika mwisho mwa msimu huu. ***(90min)***

### MBAPPE AIGOMEA PSG

HATIMA ya mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe, 22, katika klabu ya Paris St-Germain haijulikani, baada ya nyota huyo kukataa kusaini mkataba mpya. ***(Telegraph - subscription required)***

### VINICIUS KUMVUTA MBAPPE

REAL Madrid wanajiandaa kumtumia mshambuliaji wa Brazil, Vinicius Junior, 20, katika mbio za kuwania kumsajili, Kylian Mbappe wakati wa kipindi cha majira ya joto. ***(El Chiringuito, via Metro)***

### VAZQUEZ NJIA PANDA

WINGA wa Real Madrid, Lucas Vazquez, 29, ambaye mkataba wake unamalizika mwisho wa msimu huu, hajaamua kuhama hapo Santiago Bernabeu licha ya Manchester United na Chelsea kuonyesha nia ya kutaka kumnunua. ***(Sun)***

### CHELSEA YAJIPANGA

CHELSEA inapanga kuwasajili washambuliaji, Erling Braut Haaland, 20, kutoka Borussia Dortmund na Sergio Aguero wa Manchester City, mwishoni mwa msimu huu. ***(90min)***

### ANDERSEN SOKONI RASMI

LYON wameweka euro milioni 25 kama bei ya awali ya kumuuza, Joachim Andersen, 24 na rais wa Uswisi, ambaye anacheza kule Fulham kwa mkopo. Manchester United na Tottenham zimeonyesha nia ya kutaka kumsajili. ***(Metro)***

### TAKUMI ASHANGAA

WINGA wa Japan, Takumi Minamino, 26, amesema "alishangazwa" na uamuzi wa Liverpool kumtoa kwa mkopo kwenda Southampton Januari. ***(Independent)***

### WALCOTT MAMBO SAFI

SOUTHAMPTON wanajadiliana mpango wa kurefusha mkataba wa, Theo Walcott, 32, ambaye kwa sasa anacheza kwa mkopo wa msimu mzima kule Everton. ***(Southern Echo)***

### LIVERPOOL SOKONI

LIVERPOOL wamemchagua kiungo wa kati wa AZ Alkmaar, Teun Koopmeiners, 23, kujaza pengo litakaloachwa na Georginio Wijnaldum (30), mwishoni mwa msimu huu. ***(AS - in Spanish)***

## Kuogelea ya taifa kuanza leo

**Na Saada Akida**

MASHINDANO ya Taifa ya kuogelea yanatarajiwa kufanyika kuanzia leo kwenye bwawa la kuogelea la klabu ya Gymkhana Dar es Salaam na yatashirikisha wachezaji kutoka katika klabu sita za Tanzania Bara.

Mashindano hayo yanatarajia kushirikisha zaidi ya waogeleaji 90 wa Tanzania Bara na yamepangwa kufanyika kuanzia saa 2.00 asubuhi.

Waogeleaji hao watashindana katika matukio 60 kwa katika staili za Freestyle, Butterfly, Backstroke, Breaststroke na Individual Medley. Pia watashindana katika relays.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi, Hadija Shebe alisema siku ya kwanza ya mashindano hayo waogeleaji watashindana katika matukio 60 na siku ya pili washiriki watashindana katika matukio 43.

Shebe alizitaja klabu ambazo zitashiriki katika mashindano hayo kuwa ni Dar es Salaam (DSC), Taliss, Bluefins, Mwanza, FK Blue Marlins na Mis Piranhas ya Morogoro. Alisema wanatarajia kuwa na mashindano yenye upinzani na msisimko mkubwa kutokana na waogeleaji wanaoshiriki kufanya maandalizi vizuri.

"Klabu nyingi zimeleta waogeleaji wakali ambao mbali ya kuwania ushindi, pia wanapigania nafasi ya kuchaguliwa kwenye timu mbalimbali za Taifa ambazo zitashiriki mashindano ya kimataifa," alisema kiongozi huyo.

## Farouk ateuliwa Kamati ya Conifa

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limetangaza kamati maalumu itakayosimamia mashindano ya nchi zisizo wanachama wa moja kwa moja wa Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa) na CAF yatakayojulikana kwa jina la CONIFA AFRIKA, imefahamika.

Kaimu Katibu Mkuu wa ZFF, Haji Hassan 'Kibabu' aliwataja wajumbe walioteuliwa katika kamati ya mashindano hayo yatakayofanyika mwezi ujao ni pamoja na Farouk Mohammed Kareem ambaye atakuwa Mwenyekiti na Makamu wake ni Ali Saleh 'Alberto'.

Kibabu alisema Katibu wa kamati hiyo atakuwa ni Mbarouk Suleiman Othman huku wajumbe wakiwa ni pamoja na Omar Mohammed Awadhi, Seif Mohammed Seif, Salum Ali Haji, Hamza Idrissa, Salum Khamis Haji, Nasra Juma Mohammed, Hassan Hussein na Juma Mmanga Juma.

Wajumbe wengine ni Rashid Seif Mohammed, Muhsini Ali Rajab 'Kamara', Juma Suleiman Haji, Khamis Makame, Abdulamin Mohammed Juma na Zahir Rashid.

Kibabu alisema kamati hiyo ndio itakuwa na mamlaka katika usimamizi na uendeshaji wa mashindano hayo kwa mwaka huu.

# BARAZA ATAMBULISHA MFUMO MPYA KAGERA

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA mpya wa Kagera Sugar, Mkenya, Francis Baraza, amesema kwa sasa anabadilisha mfumo wa uchezaji wa kikosi chake na anaamini ndani ya muda mfupi mashabiki wa timu hiyo wataanza kuona tofauti.

**Baraza ambaye ametua Kagera Sugar kuchukua mikoba iliyoachwa na Mecky Maxime alisema hayo juzi baada ya kumalizika kwa mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Mbeya City iliyochezwa kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya na kumalizika kwa suluhu.**

Kocha huyo juzi alikiongoza kikosi hicho kwa mara ya kwanza alisema Kagera Sugar 'mpya' itaanza kuonekana na itaonyesha soka la ushindani katika michezo yake iliyobakia.

"Kwanza nawapongeza vijana. Timu zote zilicheza mchezo mzuri na kama ukiangalia kwenye msimamo timu zote haziko mahali salama. Nina wiki mbili na nusu nafanya kazi ya kubadilisha mfumo na najaribu kuleta mfumo mwingine kutokana na aina ya wachezaji nilionao," alisema Baraza.

Mkenya huyo alisema kwa sasa anaangalia namna ambavyo wachezaji wake wanavyoupokea mfumo huo.

"Najaribu kuona ni jinsi gani wanabadilika na baada ya muda mtaiona timu hii itakavyokuwa inacheza, siyo kama vile mwanzo," alisema kocha huyo wa zamani wa Biashara United.

Naye Kocha Mkuu wa Mbeya City, Mathias Lule, alisema kikosi chake kilipata shida kutokana na mfumo wa wapinzani wao, kwa sababu waliingia tofauti na walivyotegemea kuwaona wakicheza.

"Mimi namfahamu Baraza, nilijua atakuja na mfumo wa 3-5-2, ikawa hivyo, lakini baadaye kidogo akatuongezea mchezaji mwingine wa kiungo kati pale, ikatusumbua sana, maana ikanibidi nibadilishe na mimi mfumo," alisema Lule.

Baada ya sare hiyo, Kagera Sugar imefikisha pointi 26 na kukaa kwenye nafasi ya 13 huku Mbeya City imebakia katika nafasi ya 16 ikijikusanyia pointi 21.




Mshindi wa Jackpot ya SportPesa, Abdulazizi Ibrahim (wa tatu kulia), akiwa na mfano wa hundi ya Sh. milioni 521. 4 baada ya kukabidhiwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi SportPesa, Tarimba Abbas (kushoto) pamoja na baadhi ya wachezaji wa Simba na Yanga baada ya kubashiri kwa usahihi mechi zote 13 za Jackpot. Jackpot ya SportPesa ni Sh. milioni 218.3 kwa wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *SportPesa yamkabidhi Abdulaziz chake*

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya michezo ya kubashiri SportPesa imemkabidhi rasmi mshindi wa awamu ya sita wa Jackpot, Abdulaziz Ibrahim (24), mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni 521.4 ikiwa ishara ya kutimiza wajibu kama kampuni kwa washindi wake.

Baada ya mshindi huyo kutoka Sikonge mkoani Tabora kukabidhiwa zawadi yake alisema: "Nafurahi sana kwani baada ya kusubiri kwa kipindi kilichopangwa leo (jana) nimekabidhiwa rasmi fedha zangu."

"Napenda kutanguliza shukrani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu kwa kuniongoza maana nilishajaribu mara kadhaa lakini sikufanikiwa.

"Siku niliyoshinda niliweka mikeka 10 na kila mmoja Sh. 2,000, katika mikeka yote 10 mkeka namba saba ndio niliofanikiwa kushinda kwa mechi zote, mimi ni shabiki mkubwa wa Manchester United na kwa hapa Tanzania nashabikia Young Africans. Siku niliyoweka mikeka yangu niliikosesha ushindi Man U ambayo ilikuwa inacheza na Leister City kupelekea kufanikisha vizuri ushindi wangu.

"Kwa upande wa SportPesa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Tarimba Abbas alianza kwa kuwashukuru waandishi wa habari kwa kuhudhuria tukio hilo muhimu la kumkabidhi mshindi mfano wa hundi ya Sh. milioni 521.4.

"Katika ushindi wake Abdulaziz ameweza kubaki na Sh. milioni 417.1 huku akitoa Sh. milioni 104.2 kama malipo ya kodi ya zuio."

"Kila siku tunaendelea kuwa wabunifu ili kuhakikisha tunaboresha huduma na kuwafanya wateja wetu wazidi kufurahia kucheza na SportPesa," alisema Tarimba.

# Michezo

Jumamosi Aprili 10, 2021
Nipashe




Mbappe: Furaha yangu kushinda UKURASA 22



Mshambuliaji wa zamani wa Simba, Emmanuel Okwi (kushoto), akisalimiana na wachezaji wa timu hiyo, Clatous Chama (katikati) na Erasto Nyoni, alipokwenda kuwasalimia mapema jana mchana kabla ya wawakilishi hao usiku kuelekea uwanjani kuwavaa wenyeji Al Ahly katika mechi ya mwisho ya Kundi C ya Ligi ya Mabingwa Afrika. **PICHA: SSC**

## Gomes ahamishia hesabu Ligi Kuu

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kukamilisha mechi za hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes, amesema sasa hesabu zake anazihamishia kwenye michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kikosi cha Simba ambacho jana usiku kilikuwa kinavaana na vigogo wa Misri, Al Ahly mara baada ya kurejea nchini kitawakaribisha Mtibwa Sugar katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa Aprili 14, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Gomez aliliambia gazeti hili mashindano yote wanayoshiriki ni muhimu na amekiandaa kikosi chake kupambana kusaka ushindi katika kila mechi watakayocheza.

Kocha huyo alisema wanahitaji kuendelea kufanya vizuri katika mashindano ya kimataifa hivyo ushindi kwenye mechi za ligi ya nyumbani utawaongezea nguvu ya kupambana na kufanya vizuri katika kila hatua.

"Tunahitaji kufanya vizuri katika kila shindano, tumetinga hatua ya robo fainali katika Ligi ya Mabingwa Afrika, lakini bado tuna jukumu la lufanya vizuri kwenye Kombe la FA na Ligi Kuu ya Tanzania, hayo ndio malengo yetu," alisema kocha huyo raia wa Ufaransa.

Aliongeza morali waliyonayo wachezaji wake kupitia michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, inampa matumaini ya kuendelea kupata matokeo chanya katika michezo itakayofuata.

Baada ya mechi dhidi ya Mtibwa Sugar, Simba itasafiri kwenda Shinyanga kuwafuata Mwadui FC katika mechi itakayochezwa Aprili 18, mwaka huu na siku tatu baadaye itakuwa Bukoba kuwavaa wenyeji Kagera Sugar na Aprili 24, mwaka huu itawafuata Gwambina FC.

# Yanga yaiandalia dozi KMC

**Na Saada Akida**

## ●●● Lengo ni kujiimarisha katika mbio za ubingwa Ligi Kuu Tanzania Bara na...

JESHI la Yanga linatarajia kuendelea na mbio za kuwania ubingwa kwa kuwakaribisha 'Watoto wa Kinondoni' KMC FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kuanzia saa 1:00 usiku kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

**Katika mchezo huo Yanga itashuka dimbani ikiwa na kumbukumbu ya kupata ushindi wa mabao 2-1 katika mechi ya mzunguko wa kwanza iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.**

Hata hivyo katika mechi yake ya mwisho, vinara hao wa Ligi Kuu Bara walilazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya 'Maafande' wa Polisi Tanzania ambao makao makuu yao yako Moshi mkoani Kilimanjaro.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kaimu Kocha Mkuu wa Yanga, Juma Mwambusi alisema kikosi chao kipo fiti na tayari kwa ajili ya mchezo huo ambao wanafahamu utakuwa na ushindani.

Mwambusi alisema kikosi chake kimejipanga kucheza soka la kushambulia ili kuhakikisha wanashinda na kujiimarisha katika nafasi waliyopo kwenye uongozi wa ligi hiyo ya juu Tanzania Bara.

"Kila mechi kwetu ni fainali, tumejipanga vizuri, na wachezaji wote wako fiti kasoro watatu ambao hawako katika mipango yetu ya mchezo huo, ni habari nzuri kwetu kwa mshambuliaji wetu, Saido Ntibazonkiza amerejea na atakuwa miongoni mwa nyota watakaoanza,".

"Carlos Carlihnos yuko fiti ila hatokuwapo kwenye kikosi kitakachoanza lakini pia tutawakosa Farid Mussa, Yassin Mustapha ambao wanasumbuliwa na malaria, lakini Haruna Niyonzima hayuko kwenye mipango ya mchezo huo kwa sababu ameingia kambini jana (juzi) akitokea kwenye majukumu ya timu ya Taifa," alisema Mwambusi.

Nahodha wa Yanga, Lamine Moro alisema wamejipanga vizuri kwa ajili ya kupambana na kuhakikisha wanaondoka na pointi tatu muhimu katika mchezo huo na kuzikimbia timu zinazowafuata.

"Tunasikia maneno mengi nje ya uwanja ila sisi hatujali, tumejiandaa kwenda uwanjani kupambana ili kutafuta matokeo mazuri kwenye mchezo huo ambao utakuwa na ushindani mkubwa," alisema Moro.

Habibu Kondo, Kaimu Kocha Mkuu wa KMC FC, alisema wachezaji wake hawatakuwa tayari kupoteza mara mbili mechi dhidi ya Yanga katika msimu mmoja.

"Tumejipanga vizuri, tunawaheshimu wapinzani wetu, wana kikosi kizuri ila hatutaogopa kwa kuwa wanaongoza ligi, kwa sababu tumejiandaa kutafuta matokeo chanya katika mchezo huo," alisema Kondo.

Naye nahodha wa KMC FC, Juma Kaseja, alisema kazi iliyobaki ni kwao kutekeleza maelekezo waliyopewa baada ya kocha na benchi la ufundi kumaliza majukumu yao ya kuwafundisha na kuwapa mbinu za kwenda kutafuta ushindi katika mchezo huo.

"Hautakuwa mchezo rahisi, kwa sababu tumejipanga vizuri na kocha amemaliza majukumu yake, sasa kazi kubwa imebaki kwetu kuhakikisha tunapambana kutafuta matokeo chanya," alisema Kaseja.

Yanga yenye pointi 50 ndio vinara wa ligi hiyo wakifuatiwa na watani zao na mabingwa watetezi Simba wenye pointi 46, lakini wamecheza mechi tatu pungufu.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >